**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI**

# HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI

**MHESHIMIWA DKT. KHALID SALUM MOHAMED (MBM).**

## KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MEI, 2025**

## VIONGOZI WA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI - ZANZIBAR



**Mhe. Dk. Khalid Salum Mohamed (MBM)**
**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi**
**Zanzibar**



**Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Alwardy**
**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi**
**Zanzibar**



**Dkt. Habiba Hassan Omar**
**Katibu Mkuu**
**Wizara ya Ujenzi, Mawasilino na Uchukuzi Zanzibar**



**Nd. Makame Machano Haji**
**Naibu Katibu Mkuu (Ujenzi na Uchukuzi) WUMU – Zanzibar.**



**Nd. Hawwah Ibrahim Mbaye**
**Naibu Katibu Mkuu (Mawasiliano)**
**WUMU – Zanzibar.**



**Nd. Ibrahim Salehe Juma**
**Afisa Mdhamini**
**WUMU – PEMBA**

**YALIYOMO**

**YALIYOMO** .......................................................... iii
**ORODHA YA VIAMBATANISHO** .......................................vi
**A. UTANGULIZI** ........................................................ 1
**B. MAJUKUMU NA MUUNDO WA WIZARA**........................3
**C. MAFANIKIO YA UTEKELELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA MIAKA MINNE YA AWAMU YA NANE KWA SEKTA ZA WIZARA**...............................................4
**D. UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2024 HADI MACHI, 2025**...9
D.1. Ukusanyaji wa Mapato kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025. ............................................ 9
D.2. Fedha zilizopatikana kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 ....................................................... 9
D.3. Utekelezaji wa Malengo ya Programu za Wizara kwa Kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025............. 10

**PP0101 - PROGRAMU YA USAFIRISHAJI** ....................11
SP010101 - Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ............................ 11

**PP0105 - PROGRAMU YA UJENZI NA MAJENGO**.........29
SP010501 - Programu ndogo ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo.................................................... 30

**PP0103 - PROGRAMU YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)** ............................31

SP010301 - Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA....................................... 32

**PP0104 - UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI**.........35
SP010401 - Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji ..................................... 36
SP010402 - Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ................................ 37
SP010403 - Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba.............................................. 40

**E. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA MALENGO YA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA KIBAJETI ZILIZO CHINI YA WIZARA ........42**

E.1 MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI ZANZIBAR ........ 42

E.2 MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR........ 48

E.3 SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR ........ 54

E.4 SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR........ 62

E.5 MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR........ 65

E.6 BODI YA USAJILI WA WAKANDARASI. ........ 71

E.7 BODI YA USAJILI WASANIFU,WAHANDISI NA WAKADIRIAJI MAJENGO........ 73

E.8. SHIRIKA LA MAWASILIANO (ZICTIA) ........ 77

**F. MASHIRIKIANO NA TAASISI ZA MUUNGANO ........83**

**G. MCHANGO WA SEKTA BINAFSI KATIKA KUIMARISHA SEKTA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO...84**

**H. MUELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI KWA KILA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ........85**

H.1.VIPAUMBELE VIKUU VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026........ 85

H.2. MUHTASARI WA MAELEZO KWA KILA PROGRAMU NAMALENGO YANAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ........ 86

**PP0101 - PROGRAMU YA USAFIRISHAJI ........86**

SP010101 - Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ........ 87

**PP0105 - PROGRAMU YA UJENZI NA MAJENGO........92**

SP010501 - Programu ndogo ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo........ 92

**PP0103 - PROGRAMU YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA) ........95**

SP010301 - Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA ........ 95

**PP0104 - PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA .....................................................97**
SP010401 - Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji. ................................................. 97
SP010402 - Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ................................ 98
SP010403 - Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba............................................. 100

**I. HITIMISHO.........................................................................101**

**J. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026...104**

## ORODHA YA VIAMBATANISHO


KIAMBATANISHO NAMBARI 01: Ufafanuzi wa Mapato yaliyokusanywa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ...... 106

KIAMBATANISHO NAMBARI 2A: Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo Kwa Programu Kwa Kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 ................................ 107

KIAMBATANISHO NAMBARI 2B: Fedha Zilizopatikana kwa Kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 .................... 108

KIAMBATANISHO NAMBARI 3A: Utekelezaji wa Mradi wa Barabara za Mjini km 100.9 ........................................ 109

KIAMBATANISHO NAMBARI 3B: Orodha ya Barabara zilizojengwa na Kampuni ya IRIS kupitia Mradi wa Barabara za ndani zenye urefu wa km 275 ............111

KIAMBATANISHO NAMBARI 3C: Orodha ya Barabara zilizowekwa lami ya moto na Kampuni ya MAWI kupitia Mradi wa Barabara za ndani zenye urefu wa km 275....114

KIAMBATANISHO NAMBARI 4: Orodha ya Barabara zinazojengwa kupitia Mradi wa barabara zenye urefu wa Kilomita 277.7................116 .

KIAMBATANISHO NAMBARI 5: Orodha ya Barabara zinazounganisha eneo la Mangapwani zinazoendelea kujengwa......................... 117

KIAMBATANISHO NAMBARI 6A: Utekelezaji wa kazi za uandaaji wa nyaraka za Ujenzi, miezi tisa mwaka 2024/2025 ...................... 118

KIAMBATANISHO NAMBARI 6B: Utekelezaji wa kazi za Usimamizi wa Miradi ya Ujenzi kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi, 2025)............................119
KIAMBATANISHO NAMBARI 7A : Orodha ya Maeneo na Kampuni iliyojenga Minara...........................122
KIAMBATANISHO NAMBARI 7B: Idadi ya laini za simu zilizosajiliwa kwa Mikoa ya Zanzibar........................122
KIAMBATANISHO NAMBARI 7C: Minara ya simu kwa aina ya teknolojia ya urushaji wa mawimbi (2G, 3G,4G na 5G) kwa Mikoa ya Zanzibar ......... .....................................123
KIAMBATANISHO NAMBARI 7D: Hali upatikanaji wa mawasiliano katika visiwa vidogo vidogo. ................123
KIAMBATANISHO NAMBARI 8A: Wafanyakazi waliopatiwa Mafunzo ya Muda Mrefu kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 ..................124
KIAMBATANISHO NAMBARI 8B: Wafanyakazi waliopatiwa Mafunzo ya Muda Mfupi kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 ..................125
KIAMBATANISHO NAMBARI 9A: Ukaguzi wa Vyombo Vya Moto kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025.............................125
KIAMBATANISHO NAMBARI 9B: Utoaji wa Ruhusa za Njia na Usafirishaji kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 ..................125

KIAMBATANISHO NAMBARI 9C: Utoaji wa Beji za Utingo na Madereva kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025.............................. 126

KIAMBATANISHO NAMBARI 10A: Huduma za Meli............. 126

KIAMBATANISHO NAMBARI 10B: Huduma za Mizigo.......... 126

KIMABATANISHO NAMBARI 11A: Idadi ya Ndege zilizohudumiwa Katika Kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025............ 127

KIAMBATANISHO NAMBARI 11B: Kampuni za Ndege zilizotumia Kiwanja cha Ndege cha Abeid Amani Karume kwa Mwaka wa fedha 2024/2025..................... 127

KIMBATANISHO NAMBARI 11C: Idadi ya Abiria waliohudumiwa katika viwanja vya ndenge Unguja na Pemba kwa Kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025............ 130

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja kwa Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ili lipokee na kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kazi za kawaida na kazi za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

2. **Mheshimiwa Spika,** Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kushiriki katika kikao hiki cha Baraza la Wawakilishi kinachojadili Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ikiwa leo hii tunajadili utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Muelekeo wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

3. **Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa nachukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake madhubuti katika kipindi hiki cha zaidi ya miaka minne ambacho kimekuwa na maendeleo na uwekezaji mkubwa kwa Sekta zote hususan katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ili kuwaletea maendeleo wananchi wake. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa Maelekezo na Miongozo anayoitoa kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi katika kuendeleza Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ambayo inatusaidia sana kuongeza ufanisi wa kazi na kasi ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Kwa hakika Mheshimiwa Rais ametekeleza kwa vitendo ahadi alizozitoa kwa wananchi wakati wa Kampeni ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025. Kipekee tunapaswa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuiongoza vyema Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa lengo la kuleta maridhiano na kuwaunganisha Wazanzibari wote pamoja na kuhakikisha Amani, Utulivu na Mshikamano wa Kitaifa unaendelea kudumu katika nchi yetu.

4. **Mheshimiwa Spika,** Nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa namna ambavyo wamekuwa wakimsaidia Mheshimiwa Rais katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, nachukua fursa hii kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kusimamia vyema utekelezaji wa shughuli za Serikali pamoja na kuratibu vizuri shughuli zote za Baraza lako Tukufu. Vilevile, namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Dkt. Mwinyi Talib Haji pamoja na watendaji wake kwa mashirikiano yao makubwa wanayotupatia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii.

5. **Mheshimiwa Spika,** Napenda pia nikupongeze wewe binafsi kwa kuliongoza Baraza la Wawakilishi kwa kipindi chote cha miaka mitano kwa weledi, busara na hekima kubwa. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Naibu Spika kwa kukusadia katika kuliongoza vyema Baraza lako Tukufu. Vilevile, napenda kuwapongeza Wenyeviti wa Baraza pamoja na Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kusaidia kuendesha shughuli za Baraza hili.

6. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mapenzi makubwa sana natoa shukurani zangu kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati chini ya uongozi makini wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Yahya Rashid Abdalla, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Kwahani, Makamo Mwenyekiti Mheshimiwa Aza Januari Joseph kwa kutoa mashirikiano mazuri kwa Wizara hii. Tunaishukuru Kamati kwa kujadili na kuridhia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (Fungu P01) kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026. Wizara imenufaika sana na ushirikiano wa Kamati hii katika kuchambua, kushauri na kufuatilia majukumu yanayosimamiwa na Wizara hii. Tunapenda kuliarifu Baraza

lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa kikamilifu katika hotuba hii.

7. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuwashukuru Watendaji wa Ofisi ya Baraza lako Tukufu kwa ushirikiano wao wakati wote tunapotekeleza majukumu ya Wizara pamoja na wakati wa kuwasilisha taarifa mbalimbali. Tunawahakikishia kuwa, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika ili kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa na wananchi katika nyanja za kiuchumi na kijamii.

8. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwashukuru Wapiga Kura wa Jimbo langu la Uchaguzi la Donge kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kuliletea maendeleo Jimbo letu, bila kuisahau familia yangu kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu ya kulitumikia Taifa letu.

## B. MAJUKUMU NA MUUNDO WA WIZARA

9. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ina jukumu la kusimamia Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na kuandaa na kusimamia Sera, Sheria, Miongozo na kuendeleza tafiti na ubunifu unaohusiana na Sekta hizo. Aidha, Wizara inasimamia Mageuzi ya Kidijitali yanayolenga kulipeleka Taifa kwenye Uchumi wa Kidijitali.

10. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi inatekeleza majukumu hayo kupitia idara tatu (3), Ofisi kuu Pemba na Taasisi kumi na moja (11) zinazojitegemea. Idara hizo ni: - Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Idara ya Mawasiliano. Taasisi zinazojitegemea ni:- Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani, Mamlaka ya Usafiri Baharini, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Shirika la Bandari, Shirika la Meli, Shirika la Mawasiliano, Wakala wa Barabara, Wakala wa Karakana Kuu ya Magari, Wakala wa Majengo, Bodi ya

Usajili wa Wakandarasi pamoja na Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo.

## C.MAFANIKIO KWA KIPINDI CHA MIAKA MINNE YA AWAMU YA NANE KWA SEKTA ZA WIZARA.

11. **Mheshimiwa Spika,** Kabla sijatoa maelezo ya utekelezaji kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025, kwa muhtathari naomba kuwasilisha mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka minne kwa Serikali ya Awamu ya Nane kwa Sekta za Wizara kama ifuatavyo:

### Sekta ya Usafiri wa Nchi Kavu (Barabara)

12. **Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha inawapatia wananchi huduma bora za usafiri wa barabara mijini na vijini Unguja na Pemba, kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi katika ya Awamu Nane imendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya Ujenzi wa barabara ikiwemo barabara za ndani, barabara za mijini na barabara Kuu Unguja na Pemba. Katika kipindi cha miaka minne kutoka mwaka 2021/2022 hadi mwaka 2024/2025, Wizara imefanikiwa kujenga Jumla ya kilomita 321.295 kwa kiwango cha lami Unguja na Pemba. Kati ya hizo kilomita 23.8 ni barabara Kuu, kilomita 80 barabara za mijini na kilomita 217.495 ni barabara za ndani na vijijini. Aidha, jumla ya kilomita 448.28 zinaendelea kujengwa na zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

    Kutokana na mafanikio hayo, mtandao wa barabara zenye lami Zanzibar umeongezeka kutoka Kilomita 815.45 Mwaka 2021/2022 hadi kufikia Kilomita 1,023.37 Mwaka 2024/2025.

### Sekta ya Usafiri wa Anga

13. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha huduma za Usafiri wa Anga Unguja na Pemba, kwa kipindi cha miaka minne kutoka mwaka 2021/2022 hadi kufikia mwaka 2024/2025,

Wizara imefanikiwa kuaza rasmi mradi wa ujenzi wa uwanja wa Ndege wa Pemba ambao una lengo la kuongeza urefu wa barabara ya kutua na kurukia ndege (runway and taxi way), kujenga jengo jipya la abiria (Terminal Building) na miundombinu husika itakayowezesha uwanja huo kutua ndege aina ya Code C (Boeing 737-800). Ujenzi wa Uwanja huo unategemea kukamilika mwaka 2028. Aidha, Wizara imefanikiwa kuendelea na ujenzi wa Jengo la Abiria Terminal II ambalo limefikia asilimia 57 ya utekelezaji na litarajiwa kukamilika mwezi wa Januari, 2026 na litakuwa na uwezo wa kuhudumia abiria 1,300,000 kwa mwaka. Aidha, Serikali imefanikiwa kuimarisha huduma katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume kwa kushirikiana na Sekta Binafsi ikiwemo Kampuni ya SEGAP kutoka Ufaransa ambao wanaisadia kusimamia huduma za uendeshaji Viwanja kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za Anga hapa nchini. Pia, Kampuni ya Emirate leisure ambayo inaendesha biashara katika jengo jipya la TB3 pamoja na Kampuni ya Dnata inayojishughulisha na kuhudumia ndege. Kupitia Kampuni hizi uwanja wa ndege wa AAKIA umeweza kupata tuzo ya Kimataifa inayohusiana na mabadiliko ya huduma bora za chakula na vinywaji kutoka " Airport Food & Bevarage + Hospitality Conference & Awards kwenye Mkutano wake uliofanyika Bangkok nchini Thailand. Pamoja na kupata cheti cha usafirishaji wa mizigo "RA3" kutoka Uwanja wa AAKIA kwenda Nchi za Ulaya.

Aidha, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume umepata Tunzo ya kuwa Kiwanja Bora Barani Afrika kinachohudumia Abiria chini ya Milioni Mbili kwa mwaka iliyotolewa Mwaka 2023. Tunzo hii hutolewa na Baraza la Viwanja vya Ndege Duniani (Airport Council International - ACI) kwa Viwanja vya ndege ambavyo ni Wanachama wa Baraza hilo wanaojiunga katika Programu maalum ya kupima uwezo wa utoaji wa Huduma kwa abiria katika Viwanja vyao.

14. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miaka minne, abiria wanaoingia na kutoka Zanzibar kwa kutumia Viwanja vya Ndege vya Zanzibar wameongezeka kutoka abiria 1,265,106

mwaka 2021/2022 hadi kufikia abiria 2,004,380 mwaka 2024/2025. Ongezeko hili linatokana na kuwepo kwa huduma bora katika Viwanja vya Ndege vya Zanzibar pamoja na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi nchini.

Aidha, Mashirika ya ndege yanayokuja Zanzibar yanaendelea kuongezeka kutoka Mashirika 60 kwa mwaka 2021/2022 hadi kufikia Mashirika ya Ndege 86 mwaka 2024/2025. Baadhi ya Mashirika makubwa yanayokuja Zanzibar ni Edelweis na Eurowings kutoka ujerumani, Etihad kutoka falme za kiarabu (UAE), Fly Saf Air kutoka Afrika Kusini, Air France kutoka ufaransa, High fly kutoka Ureno, Jambo jet kutoka Kenya na World 2 fly kutoka Spain. Pia, Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar kilipata alama “A” kwenye ukaguzi wa masuala ya ulinzi na usalama wa Viwanja vya Ndege uliofanyika Mwezi wa Mei 2023 na Wakaguzi kutoka Shirika lenye dhamana ya usimamizi wa Usafiri wa Anga Duniani ICAO. Mafanikio haya yanatokana na Serikali kuimarisha huduma za ulinzi na usalama katika viwanja vya Ndege vya Zanzibar.

**Sekta ya Usafiri wa Baharini**

**15. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha Sekta ya Usafiri wa Baharini, kwa kipindi cha miaka minne kutoka mwaka 2021/2022 hadi kufikia mwaka 2024/2025,Wizara imefanikiwa kuingia Mkataba na Kampuni mbali mbali za Kimataifa katika Ushirikiano na Sekta Binafsi nchini kwa lengo la kuziendesha Bandari mbali mbali ambapo Bandari ya Makontena Malindi imekabidhiwa Kampuni ya ZMT / AGL, Kampuni ya MJ group imekabidhiwa bandari ya Fumba na Mkoani kwa ajili uendeshaji, Kampuni ya ZF Devco imekabidhiwa ujenzi wa bandari ya abiria Maruhubi pamoja na uendeshaji katika bandari ya abiria Malindi, Pia, kuna Wawekezaji mbali mbali katika bandari jumuishi ya Mangapwani ambao wamewekeza katika masula ya mafuta na gesi.

16. **Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kuwepo kwa ushirikiano wa uendeshaji wa bandari zetu na Sekta Binafsi kumepelekea kuongezaka ufanisi katika shughuli za bandari. Kwa upande wa Bandari ya Malindi, Serikali imefanikiwa kuongeza ufanisi ambapo imeweza kupunguza muda wa meli kusubiri ukutani kutoka siku arubaini (40) kwa mwaka 2021/2022 hadi kufikia siku nane (8) kwa mwaka 2024/2025. Aidha, shughuli za ushushaji na upakiaji wa makontena na mizigo kichele zimeongezeka kutoka tani elfu kumi na nne (14,000) mwaka 2021/2022 kwa saa hadi kufikia tani thalathini na mbili (32,000 tons) mwaka 2024/2025 kwa saa. Aidha, katika kuhakikisha msongamano wa Makontena unapunguwa katika Banadari ya Malindi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejenga bandari kavu katika eneo la Maruhubi pamoja na ujenzi wa Bandari ya Fumba ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wafanyabiashara pamoja na kupunguza msongamano wa Makontena katika Bandari ya Malindi.

17. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha huduma za usafiri wa Bahari, Wizara kwa kipindi cha miaka minne imefanikiwa kuendelea na ujenzi wa bandari ya abiria Maruhubi kwa kushirikiana na Kampuni ya ZF Devco pamoja na Kampuni ya MJ kwa ujenzi wa gati katika Bandari ya Fumba. Pia, Wizara imekamilisha upembuzi yakinifu na Mpango Mkuu (Master Plan) wa ujenzi wa Bandari ya Wete, kuimarisha Bandari ya Mkoani ikiwemo kutoa huduma za meli za makontena, kujengwa Bandari kavu, kuweka baji kwa ajili ya boti za mwendo kasi, kukamilisha ujenzi wa Bandari ya Shumba Mjini, Micheweni itakayo wezesha safari baina ya Pemba, Mombasa na Tanga. Aidha, Serikali imeanza ujenzi wa bandari ya Makontena Mangapwani.

18. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imeanza ujenzi wa boti mbili za mwendo wa kasi zitakazofanya kazi baina ya Unguja, Pemba, Tanga na Dar es Salaam. Boti hizo zinajengwa na Kampuni ya Synergy Shipbuilder kutoka India na ujenzi wa boti hizo unafanyika nchini India. Boti hizi zinatarajiwa kuwasili nchini Mwezi wa Juni, 2026 na zitakuwa na uwezo wa kuchukuwa abiria 650 kwa kila moja.

## Sekta ya Ujenzi

19. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha Sekta ya Ujenzi, Wizara kwa kipindi cha miaka minne imefanikiwa kusajili jumla ya Wandarasi 293. Kati ya hao Wakandarasi 273 ni Wakandarasi wa ndani na Wakandarasi 20 ni kutoka nje ya nchi. Aidha, jumla ya wataalamu wa ujenzi (Professional) 265 wamesajiliwa hapa Zanzibar na jumla ya Kampuni za Ushauri 141 zimesajiliwa kwa kipindi hicho. Vile vile, Wizara imefanikiwa kutoa huduma za Ushauri Elekezi (Usimamizi) katika miradi ya Serikali na jumla ya miradi 110 imesimamiwa Unguja na Pemba.

## Sekta ya Mawasiliano

20. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha Sekta ya Mawasiliano, Wizara inaendelea kuimarisha miundombinu ya Mawasiliano kwa kulaza Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano kutoka Kilomita 450 kwa mwaka 2021/2022 hadi kufikia kilomita 1,500 kwa mwaka 2024/2025. Lengo ni kuhakikisha kuwa huduma za mawasiliano ikiwemo huduma za mtandao zinapatikana kwa urahisi Unguja na Pemba ili kukuza uchumi wa kidijital Zanzibar. Aidha, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (SMZ) ikishirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (SJMT) kwa kipindi cha miaka minne imefanikiwa kujenga minara ya mawasiliano ya simu 42 katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba ambapo imeifanya Zanzibar hadi kufikia mwaka 2024/2025 kuwa na minara ya Mawasiliano 474. Ujenzi wa minara hiyo, umeongeza upatikanaji wa mawasiliano ya sauti (voice) kwa kutumia simu za mkononi kufikia asilimia 100 katika maeneo yote yenye makaazi ya watu hapa Zanzibar.

21. **Mheshimiwa Spika,** Utoaji wa huduma za mawasiliano ya simu kwa kusafirisha mawimbi kutumia teknolojia ya 2G, 3G, 4G na 5G imeongezeka kutoka mitambo 1,545 mwezi Juni 2024 hadi kufikia mitambo 1741 mwezi Machi 2025. Hali hii imepelekea kuimarika kwa huduma za mawasiliano

nchini. Aidha, kuimarika kwa miundombinu ya mawasiliano kumepelekea ongezeko la watumiaji wa huduma hizo ambapo takwimu zinaonesha kuwa, laini za simu zilizosajiliwa Unguja na Pemba zimeongezeka kutoka 601,132 Mwezi Juni, 2022 hadi kufikia laini 1,058,516 Mwezi Machi, 2025 sawa na ongezeko la asilimia 76.

22. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanikiwa kuweka Anuani za Makaazi katika shehia zote 388 zilizopo Unguja na Pemba. Anuani za Makaazi zipatazo 528,417 zimesajiliwa katika mfumo wa National Physical Addressing (NaPA), ambapo makaazi yote Unguja na Pemba yamepewa anuani hizo. Aidha, Serikali imefanikiwa kutenga na kutangaza maeneo huru ya uwekezaji Kidijitali Zanzibar (Zanzibar Digital Freezone) yaliyopo Fumba ambapo Serikali itajenga Mji wa TEHAMA (Zanzibar Cyber City).

## D.UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2024 HADI MACHI, 2025

### D.1. Ukusanyaji wa Mapato kwa Kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025

23. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 3,792,926,000** na kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 3,120,750,000**. Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **Shilingi 2,690,032,880** zimekusanywa sawa na asilimia **86.1** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **70.9** kwa makadirio ya mwaka. **Kiambatanisho namba 1 kinatoa ufafanuzi**.

### D.2. Fedha zilizopatikana kwa Kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025

24. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Programu zake kuu nne (4) kwa Mwaka wa

Fedha 2024/2025, iliidhinishiwa na Baraza la Wawakilishi kutumia jumla ya **Shilingi 1,107,123,874,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 3,225,000,000** ni mshahara, **Shilingi 3,288,400,000** ni matumizi ya uendeshaji wa Ofisi, **Shilingi 29,394,300,000** ni Ruzuku na **Shilingi 1,071,216,174,000** ni kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 Wizara ilipanga kutumia jumla ya **Shilingi 796,418,347,974**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,418,749,992** ni mshahara, **Shilingi 2,583,643,479** kwa kazi za kawaida, **Shilingi 26,152,985,194** ni ruzuku na **Shilingi 765,262,969,309** kwa kazi za maendeleo.

**25. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Mwezi wa Machi, 2025 jumla ya **Shilingi 466,972,287,270.48** zimepatikana sawa na asilimia **58.6** ya makadirio ya bajeti kwa kipindi cha miezi tisa na asilimia **42** wa makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,124,577,714.4** ni mshahara sawa na asilimia 87.8 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **65.9** ya makadirio ya mwaka, **Shilingi 781,904,950** ni kazi za kawaida sawa na asilimia **30** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **23.7** kwa mwaka, **Shilingi 16,325,618,370** ni Ruzuku kwa taasisi zilizomo ndani ya Wizara sawa na asilimia **62.4** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **55.5** ya makadirio ya mwaka na **Shilingi 447,740,186,235 .98** ni kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia **58.5** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **41.7** ya mwaka. **Kiambatanisho namba 2A na 2B kinatoa ufafanuzi**.

## D.3. Utekelezaji wa Malengo ya Programu za Wizara kwa Kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025

**26. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha, 2024/2025, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imetekeleza kazi zake kupitia Programu kuu nne (4) na Programu ndogo sita (6). Utekelezaji wa malengo ya programu hizo kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 ni kama ifuatavyo: -

## PP0101 - PROGRAMU YA USAFIRISHAJI

**27. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu na huduma za usafiri zilizo bora, salama na endelevu na zitakazoleta matokeo bora katika Sekta ya Uchukuzi. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Programu ya Usafirishaji ina Programu ndogo moja (1) ambayo ni Programu ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji.

### SP010101 - Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji.

**28. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Wakala wa Karakana Kuu ya Magari na Wakala wa Barabara Zanzibar. Wizara kupitia taasisi zinazosimamia programu hii imetekeleza mambo yafuatayo: -

### IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

**29. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ina jukumu la kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia programu hii ilipanga kusimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi ifuatayo:-

a. **Mradi wa Barabara za Mjini Unguja Zenye Urefu wa Kilomita 100.9:** Wizara inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Barabara za Mjini zenye urefu wa kilomita 100.9 unaojumuisha ujenzi wa barabara za juu (Fly overs) katika eneo la Amani na Mwanakwerekwe. Mkataba wa Ujenzi wa mradi huu ulisainiwa tarehe 06 Agosti, 2022 kwa gharama ya Dola za Kimarekani 116,131,442.96 sawa na Shilingi 268,456,411,432.91 na kuanza rasmi utekelezaji wake tarehe 1 Disemba, 2022 na umepangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miezi 36. Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya Kilomita 80 kati ya

100.9 sawa na asilimia 80 zimejengwa **Kiambatanisho Nambari 3A. Kinahusika**. Ujenzi wa barabara hizi unatekelezwa na Kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) kutoka nchini China na Msimamizi wa ujenzi ni Kampuni ya Dar-al-handasah kutoka Lebanon. Fedha za utekelezaji wa mradi huu zinatolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

30. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha, 2024/2025, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 112,092,000,000** kutoka Serikalini na hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **Shilingi 79,963,586,189.98** zimepatikana sawa na asilimia **71.3**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 72,714,225,793** ni malipo ya Mkandarasi, **Shilingi 1,118,448,508** ni malipo ya Mshauri Elekezi na **Shilingi 6,130,911,889** ni malipo ya fidia kwa wananchi waliopisha mradi huu.

b. **Mradi wa Barabara za Ndani Zenye Urefu wa Kilomita 275.9 Unguja na Pemba:** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupita Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ilisaini Mkataba na Kampuni ya IRIS/ASER tarehe 22 Novemba, 2021 wa ujenzi wa barabara za ndani kwa kiwango cha lami aina ya Chip Seal kwa gharama ya Dola za Kimarekani 80,300,000 bila VAT sawa na Shilingi 185,179,027,000. Aidha, Wizara ilisaini Mkataba na Kampuni ya MAWI tarehe 18 Machi 2024 kwa ajili ya kuziwekea lami ya moto (Hot Mix Asphalt Concrete) barabara hizo zenye urefu wa Kilomita 275.9 (Unguja 140.95 km na Pemba 134.95 km) kwa gharama ya Dola za Kimarekani 79,167,226 bila ongezeko la thamani (VAT) sawa na Shilingi 202,421,888,487.14. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kazi za ujenzi zinasimamiwa na Wakala wa Barabara Zanzibar (ZANROADS).

Utekelezaji wa mradi huu hadi Machi, 2025 umefikia asilimia 82.02, ambapo jumla ya Kilomita 219.75 zimejengwa kwa hatua mbali mbali za kifusi na lami Unguja na Pemba. Kati ya hizo, Kilomita 88.01

zimekamilika kwa hatua za kifusi na kilomita 131.74 zimekamilika kwa kiwango cha lami (Unguja 103.10km na Pemba 28.64km), ambapo kwa ujumla kazi ya uwekaji wa lami ya moto inayotekelezwa kupitia Kampuni ya MAWI Construction, hadi mwezi Machi, 2025, imefikia asilimia 47.7. **Kiambatanisho namba 3B na 3C** vinahusika.

31. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 45,600,000,000** kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **Shilingi 79,226,135,149.25** zimetumika sawa na asilima **174** ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo **Shilingi 28,745,273,961.83** ni malipo ya Mkandarasi Kampuni ya IRIS, **Shilingi 50,130,186,068.42** ni malipo ya Mkandarasi kwa Kampuni ya MAWI na **Shilingi 350,675,119** ni malipo ya fidia kwa wananchi pamoja uhamishaji wa miundombinu ya umeme Pemba. Ziada ya fedha zilizotumika zilihaulishwa kutoka mradi wa Barabara kuu.

c. **Barabara Kuu za Zanzibar:** Mradi huu unajumuisha ujenzi wa barabara kuu za Unguja na Pemba zikiwemo Tunguu – Makunduchi Kilomita 48, Fumba – Kisauni Kilomita 12, Mkoani - Chake Chake Kilomita 43.5 pamoja na barabara ya Chake – Wete kilomita 22.1. Utekelezaji wa Mradi huu hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Machi, 2025 ni kama ifuatavyo: -

i. **Ujenzi wa Barabara ya Tunguu – Makunduchi 48km na Fumba – Kisauni 12km:** Barabara hizi zitajengwa na Kampuni ya Mwananchi Engineering Contructing Company Limited - MECCO kwa mkopo kutoka “United Kingdom Export Finance – UKEF”, kwa gharama ya Euro 137,461,389.58 sawa na Shilingi 378,148,035,051.20. Wizara imesaini Mkataba wa Ujenzi tokea mwezi wa Aprili, 2024. Utekelezaji wa mradi hadi kufikia Mwezi Machi, 2025, Mkandarasi anasubiria kuingiziwa Fedha ya Awali (Advance Payment) ambazo hulipwa na Wahisani kupitia

Benki ya "Deutch Bank – London" kwa ajili ya kuanza kazi rasmi.

ii. **Ujenzi wa Barabara ya Mkoani – Chake km 43.5:** Ujenzi wa Barabara ya Mkoani – Chake yenye urefu wa Kilomita 43.5 unatekelezwa na Kampuni ya PROPAV Infrastructures kwa mkopo kutoka "United Kingdom Export Finance (UKEF)" kwa gharama ya Euro 93,337,402.83 sawa na Shilingi 256,765,594,941.16. Mkataba wa Ujenzi wa Barabara hii ulisainiwa Mwezi wa Septemba, 2022 baina ya Mjenzi Kampuni ya "Propav Infrastructures" na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2025, Mkandarasi anasubiri kuingiziwa Fedha ya Awali (Advance Payment) zinazolipwa na Wahisani kupitia Benki ya "Deutch Bank - London" kwa ajili ya kuanza kazi rasmi. Msimamizi wa Ujenzi ni Kampuni ya Dar al Handasah Consultants (Shair and Partners).

iii. **Ujenzi wa Barabara ya Chake - Wete 22.1km:** Wizara inaendelea na ujenzi wa barabara ya Wete – Chake yenye urefu wa Kilomita 22.1. Mkataba wa Ujenzi wa barabara hii ulianza rasmi mwezi wa Februari, 2022 na ulipangwa kukamilika mwezi Agosti, 2024. Muda wa awali wa utekelezaji wa mradi huu ulikuwa ni miezi 30. Kazi za ujenzi wa barabara hii zinatekelezwa na Kampuni ya MECCO kutoka Dar - es – Salaam na kazi za ujenzi zinasimamiwa na Mshauri Elekezi Kampuni ya Dar al Handasah. Aidha, Barabara hii inajengwa kwa kutumia fedha za Mkopo kutoka Washirika wa Maendelea BADEA na SAUDI FUND pamoja na mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla Shilingi 23,578,031,917 kwa ajili ya ujenzi na Shilingi 3,013,080,000 kwa ajili ya kazi za usimamizi wa mradi. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina jukumu la fidia za wananchi wanaotakiwa kupisha kazi za ujenzi huo.

Mradi huu ulilazimika kuombewa kuongezewa muda wa miezi mitano (5) na baadae miezi tisa (9) na kutarajiwa kukamilika tarehe 30/10/2025 badala ya tarehe 14/08/2024, sambamba na kuongezeka kwa gharama za ziada kutoka Shilingi 23,578,031,917 hadi Shilingi 26,618,162,917 na kufanya ongezeko la Shilingi 3,040,131,000. Sababu kubwa ya ongezeko la muda na gharama linatokana na kwamba, awali Mradi huu ulipangwa kufanyiwa ukarabati wa kawaida (Rehabilitation) barabara ya Wete – Chake, hata hivyo wakati wa ujenzi ilibainika kuwa barabara hiyo inahitaji kujengwa upya (Re-Construction) kulingana na hali ya Barabara iliyopo pamoja na mazingatio ya hali ya udongo wa eneo la ujenzi. Utekelezaji wa Mradi huu hadi kufikia mwezi Machi 2025 umefikia asilimia 60 na jumla ya Shilingi 2,165,671,343.93 zimetumika sawa na asilimia 43 ya makadirio ya bajeti.

iv. **Ujenzi wa Barabara zenye urefu wa Kilomita 277.7:** Mradi huu unajumuisha ujenzi wa barabara za Unguja na Pemba pamoja na ujenzi wa daraja la Uzi. Muda wa utekelezaji wa mradi huu ni miezi 36 na kazi za ujenzi zinatekelezwa na Kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) kwa gharama ya Dola za Kimarekani 308,634,767.73, sawa na Shilingi 737,637,094,874.7 na kusimamiwa na Mshauri Elekezi Dar Al Handasah kutoka nchini Lebanon. Utekelezaji wa Mradi huu, umeanza kwa ujenzi wa barabara za Kizimbani – Kiboje Kilomta 7.2, Kitogani – Paje Kilomita 10.6 na barabara ya Uzi – Ng'ambwa kilomita 6.5. pamoja na Daraja lenye urefu wa Kilomita 2.2. Ujenzi ulianza rasmi mwezi Novemba, 2024 ambapo hadi kufikia mwezi wa Machi, 2025 kazi zilizokamilika ni uwekaji wa lami Kilomita 7.2 kwa barabara ya Kizimbani - Kiboje na uwekaji wa kifusi tabaka tofauti kwa barabara ya Kitogani – Paje na barabara ya Uzi – Ng'ambwa pamoja na kukamilisha michoro ya Daraja la Uzi. Kwa ujumla ujenzi wa barabara hizi umefikia asilimia 41.9 ya utekelezaji. **Kiambatanisho**

**Namba 4 kinahusika**. Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya Shilingi 32,629,221,164.49 zimepatikana. Kati ya fedha hizo Shilingi 17,296,039,794 ni malipo ya Mkandarasi ya Barabara ya Kizimbani - Kiboje na Shilingi 15,333,181,370.49 ni malipo ya Mkandarasi ya Barabara ya Jozani - Charawe – Ukongoroni.

v. **Ujenzi wa Barabara zinazounganisha eneo la Mwangapwani na Nyenginezo:** Mnamo tarehe 16 Oktoba, 2024 Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi imeingia Mkataba na Kampuni ya Orkun Group Zanzibar Limited kwa ajili ya Ujenzi wa Barabara zinazounganisha Bandari ya Mangapwani na maeneo mengine awamu ya pili zenye urefu Kilomita 113.8 kwa muda wa miezi 15 na wenye gharama za Dola za Kimarekani 93,092,500. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025, kazi zilizofanyika ni usanifu na ujenzi wa barabara kwa hatua mbalimbali. Mradi huu hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Machi, 2025 umefikia asilimia 20 ya utekelezaji. **Kiambatanisho Nambari 5 kinahusika**. Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya Shilingi 44,405,600,880 zimetumika ikiwa ni malipo ya Mkandarasi na Shilingi 326,277,610 zimetumika kwa ajili ya malipo ya fidia za wananchi.

32. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ujenzi wa Barabara kuu ulipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 311,766,552,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 115,540,531,000** ni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, **Shilingi 5,000,000,000** ni kutoka BADEA na SAUD FUND, **Shilingi 113,226,021,000** ni kutoka kwa UKEF na **Shilingi 78,000,000,000** ni kutoka Exim Benki ya China. Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya **Shilingi 79,526,770,998.42** zimepatikana sawa na asilimia 25.5 ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,165,671,343.93** zinatoka kwa BADEA na SAUDI FUND, na **Shilingi 77,361,099,654.49** ni kutoka Serikalini kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi na fidia.

d. **Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usafiri wa Umma Zanzibar.** Mradi huu unatekelezwa na Mshauri Elekezi, Kampuni ya IDOM Consulting, Engineering, Architecture ya Hispania kupitia Ruzuku kutoka Serikali ya Hispania. Kampuni hii iliingia Makubaliano na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi tarehe 17 Julai, 2023 na kuanza kazi rasmi mwezi Febuari, 2024. Muda wa utekelezaji wa mradi huu ni miezi 18 wenye gharama ya jumla ya Euro 1,179,278.88 sawa na Shilingi 3,568,816,296. Matokeo yanayotarajiwa kupatikana kutokana na utafiti huu ni pamoja na Andiko la Mradi (Feasibility Study) linalotoa mapendekezo ya namna ya kuwa na mfumo wa kisasa wa usafiri wa umma. Aidha, matokeo hayo yatasaidia kupatikana kwa Sera ya Usafiri na Usafirishaji ya Zanzibar na Mpango Mkuu wa Usafiri na Usafirishaji Zanzibar, ambapo hadi kufikia Machi, 2025, Mshauri ameshawasilisha ripoti ya mapendekezo ya mfumo wa daladala (Proposed Reorganisation of the Daladala System) kwa Unguja na Pemba. Kwa ujumla mradi umefikia asilimia 77.7 ya utekelezaji.

33. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mradi ulipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 1,941,713,000** kutoka kwa Mhisani na hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya **Shilingi 1,013,696,552** zimepatikana sawa na asilimia **52.2** ya makadirio ya bajeti.

e. **Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba:** Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba unatekelezwa na Kampuni ya Pemba Airport Construction Consortium (PROPAV Infrastructures) kwa mkopo kutoka "United Kingdom Export Finance (UKEF)" wenye gharama ya Euro 170,000,000 sawa na Shilingi 467,659,800,000. Mkataba wa Ujenzi ulisainiwa tarehe 04 Januari, 2023 baina ya Mjenzi na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Utekelezaji wa mradi huu ulianza rasmi mwezi Novemba, 2024. Hadi kufikia Machi, 2025, kazi zinazoendelea ni kukamilisha michoro na usanifu

(Detailed Drawings and Designs) pamoja na ujenzi wa ambi ya Mkandarasi (Constractor's Camp site). Kazi nyengine zilizofanyika ni muendelezo wa zoezi la ulipaji wa fidia za wananchi watakaopisha eneo la ujenzi wa mradi (Project Construction area) pamoja na eneo la ujenzi wa Kambi ya Mkandarasi (Contractor's camp site) ambapo jumla ya Shilingi 12,945,496,209 zimetumika kuwalipa wananchi wapatao 957.

34. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 101,391,149,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 9,500,000,000** ni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na **Shilingi 91,891,149,000** ni kutoka kwa Mfadhili. Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **Shilingi 20,461,578,480** zimepatikana sawa na asilimia **20.1** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 12,896,178,750** ni kutoka kwa Mfadhili UKEF ikiwa ni malipo ya Mkandarasi, **Shilingi 5,038,875,000** zimelipwa kwa Mshauri Elekezi na **Shilingi 2,526,524,730** ni malipo ya fidia kwa wananchi waliopisha mradi.

f. **Mradi wa Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria la Terminal II:** Ujenzi wa Jengo Jipya la Pili la Abiria (TB2) umetokana na uchakavu wa miundominu kwenye Jengo la Pili la Abiria (TB2) hali iliyopelekea kuwa na malalamiko mengi ya watumiaji wa jengo hilo, Serikali imeingia Mkataba na Kampuni ya Esteem Enterprises kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo na tayari Awamu ya Mwanzo ya ujenzi wa jengo ilianza rasmi mwezi Januari, 2024. Jengo hili litakapokamilika litakuwa na uwezo wa kuhudumia abiria 1,300,000 kwa mwaka. Ujenzi wa jengo hili limefikia asilimia 57 ya utekelezaji na linatarajiwa kukamilika mwezi wa Januari, 2026.

35. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mradi ulipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 26,000,000,000** kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya **Shilingi 17,930,324,525.28** zimepatikana sawa na asilimia **66.5** kwa ajili ya kumlipa Mkandarasi.

**g.Mradi wa Ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani**

i. **Ujenzi wa Bandari ya Mangapwani:** Serikali imepanga kujenga Bandari Jumuishi katika eneo la Mangapwani itakayohudumia makontena na mizigo ya kichele, mafuta na gesi pamoja na Chelezo. Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imeingia Mkataba na Kampuni ya China Harbour Engineering Company (CHEC) mwezi wa Februari, 2024 kwa ajili ya ujenzi wa bandari hiyo. Mradi huu utachukuwa muda wa miezi 36 hadi kukamilika kwake. Ujenzi wa Bandari ya Mangapwani umeanza, kwa sasa Mkandarasi anaendelea na kazi za awali ikiwemo utafiti wa udongo (Geotechnical Investigation), usanifu na kuandaa michoro (Detailed Design) pamoja na ujenzi wa Kambi ya Mkandarasi. Aidha, ujenzi wa Bandari hii hadi kukamilika kwake unatarajiwa kutumia jumla ya Dola za Kimarekani 350,446,043.57. Hadi kufikia Machi, 2025, Mkandarasi amelipwa Shilingi 125,640,096,802.73 ikiwa ni malipo ya Fedha za Awali (Advance Payment).

ii. **Ujenzi wa Barabara katika Eneo la Bandari ya Mangapwani:** Wizara inaendelea na ujenzi wa Barabara katika eneo la Mradi wa Bandari Jumuishi ya Mangapawani yenye urefu wa kilomita 12. Kazi za ujenzi wa barabara hiyo zinatekelezwa na Kampuni ya ORKUN Group ambayo imepewa Mkataba wa miezi kumi na nane (18) kwa gharama za Dola za Kimarekani 35,572,500. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya kilomita 5.8 zenye Barabara mbili (Dual carriage way) zimeshajengwa kwa kiwango cha lami sawa na asilimia 45. Kazi za ujenzi zinaendelea na Mkandarasi ameshalipwa jumla ya Dola za Kimarekani 15,750,000 sawa na asilimia 44.27 ya malipo yote. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) kwa mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya Shilingi 12,629,021,550 zimetumika kati ya fedha hizo Shilingi 2,770,776,000 ni kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi waliopisha ujenzi na jumla Shilingi 9,858,245,550 ni malipo ya Mkandarasi.

iii. **Ujenzi wa Nyumba za Fidia katika eneo la Mangapwani na Bumbwini:** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeingia Mkataba na Kampuni ya ORKUN Group kwa ajili ya Ujenzi wa nyumba 370 za fidia ambazo zitajengwa katika eneo la Bumbwini na Mangapwani kwa muda wa miezi 18. Mradi huu utagharimu jumla ya Dola za Kimarekani 23,994,750 na jumla ya Dola za Kimarekani 17,700,000 zimeshalipwa sawa na asilimia 64.2. Hadi kufika Machi, 2025, nyumba 100 zimekamilika na nyumba 185 zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi (finishing work) na nyumba 85 zipo katika hatua za awali za ujenzi wa misingi na kuta. Kwa ujumla Mradi huu umefikia asilimia 64 ya utekelezaji. Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya Shilingi 29,151,113,330.27 zimetumika kati ya fedha hizo Shilingi. 29,133,513,330.27 ni malipo ya Mkandarasi na Shilingi. 17,600,000 ni malipo ya fidia kwa wananchi waliopisha Mradi.

36. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha, 2024/2025, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 257,539,960,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 157,539,960,000** kutoka Serikalini na **Shilingi 100,000,000,000** ni Mfadhili. Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya **Shilingi 167,420,231,683** zimepatikana sawa na asilimia **65** ya makadirio ya bajeti. Fedha hizi zimetolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

h. **Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Abiria Maruhubi.** Mradi huu umeanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2024/2025. Mradi una lengo la kujenga bandari mpya Maruhubi ili kuimarisha huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo katika visiwa vya Unguja na Pemba, Tanzania Bara na Maeneo mengine. Mradi utahusisha ujenzi wa gati ya abiria na gati ya mizigo (RoRo) katika eneo hilo. Mradi unatarajiwa kutekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Kampuni ya ZF DEVCO na unatarajiwa kutekelezwa kwa muda wa miezi thelathini na sita. Kazi ya ujenzi wa gati ya abiria na mizigo (RoRo) inaendelea na hadi kufikia Machi, 2025 imeshafikia asilimia 30 ya utekelezaji.

37. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 127,500,000,000** kutoka kwa Kampuni ya ZF Devco na jumla **Shilingi 18,000,000,000** zimetumika sawa na asilimia **14.1** ya makadirio ya mwaka.

38. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 1,065,216,174,000** kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **572,943,683,000** ni mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na **Shilingi 492,272, 491,000** ni mchango kutoka Serikalini.

Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **Shilingi 445,542,323,577.98** zimetumika sawa na asilimia **41.8** ya makadirio. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 16,075,546,645.98** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia **2.8** ya makadirio na **Shilingi 429,466,776,932** ni fedha zilizotolewa na Serikali sawa na asilimia **87** ya makadirio ya bajeti.

## WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR

39. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Barabara Zanzibar kupitia Programu Ndogo ya Usimamzi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ina jukumu la kuimarisha mtandao wa barabara Zanzibar kwa kuzijenga na kuzifanyia matengenezo barabara mbalimbali za Unguja na Pemba ili ziweze kupitika kwa usalama kwa muda wote. Aidha, Wakala wa Barabara Zanzibar ina jukumu la kujenga na kutunza barabara za Unguja na Pemba pamoja na kutoa huduma za usimamizi na ushauri wa kitaalamu kwa Wakandarasi wanaojenga na kutekeleza miradi ya barabara Zanzibar.

40. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara Zanzibar kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 imefanikiwa kuzijenga na kufanyia matenegenezo barabara mbalimbali pamoja na

kuimarisha mazingira ya usafi kwenye miundombinu ya kupitishia maji ya mvua kwa barabara za Unguja na Pemba kama ifuatavyo:-

a. **Ujenzi wa Barabara mbalimbali za ndani zenye urefu wa km 6.7 kwa kiwango cha lami.** Wakala wa Barabara Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ilipanga kujenga barabara mbalimbali za ndani zenye jumla ya urefu wa kilomita 6.6 kwa kiwango cha lami zikijumuisha barabara ya Chuo kikuu cha Abrahman Al Sumait km 0.85, Mwakaje (selemu) – Mbuzini km 3,5 Barabara ya Chuo cha Karume (KIST) km 0.15 pamoja na maegesho kwenye Hanga la ndege katika Taasisi ya Sayasi na Teknolojia ambayo ina urefu wa mita 30 kwa mita 40 upana, Barabara ya Mahakama Kuu Tunguu – Istiqama km 0.9 na Barabara ya Kisauni – Mbuyuni km 1.2 Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025, Wakala wa Barabara imefanikiwa kukamilisha kwa asilimia 95 ujenzi wa barabara za ndani ya Chuo Kikuu cha Al Sumait zenye jumla ya urefu wa kilomita 0.85 kwa kiwango cha lami, Ujenzi wa barabara ya Kisauni – Mbuyuni kwa kiwango cha zege yenye urefu wa km 1.2 imekamilika kwa asiliamia 93. Aidha, barabara ya Mahakama Kuu Tunguu- Istiqama yenye urefu wa km 0.9 inaendelea na ujenzi hadi kufikia Machi, 2025 utekelezaji wa barabara hii umefikia asilimia 70. Barabara ya Mwakaje (Selemu) – Mbuzini yenye urefu wa km 3.5 inaendelea na ujenzi hadi Machi 2025, utekelezaji wa barabara hii umefikia asilimia 67.

   Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ujenzi wa barabara hizi zilipangiwa kutumia jumla ya Shilingi 5,624,482,850 na hadi kufikia Machi 2025 jumla ya Shilingi 2,257,044,931 zimepatikana sawa na asilimia 40 ya makadirio ya bajeti.

b. **Ujenzi wa Barabara ya Mchangani (dunga) - Msikitini km 1.1km kwa Kiwango cha Lami.** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wakala wa Barabara Zanzibar ilipanga kujenga barabara ya Mchangani (Dunga) – Msikitini yenye urefu wa Kilomita 1.1 kwa kiwango cha

lami na hadi kufikia Machi, 2025 ujenzi wa barabara hii umefikia asilimia 85 ya utekelezaji.

Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya Shilingi 706,142,544 na hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya Shilingi 706,142,544 zimepatikana sawa na asilimia 100 ya makadrio ya mwaka

c. **Ujenzi wa Barabara za Ndani za Kizimkazi Zenye Jumla ya Urefu wa Kilomita 6.59 kwa Kiwango cha Lami:** Wakala wa Barabara Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ilipanga kujenga barabara za ndani za Kizimkazi zenye jumla ya urefu wa Kilomita 6.59 kwa kiwango cha lami ambapo kazi hiyo imekamilika kwa asilimia 100. Mradi huu umejumuisha ujenzi wa barabara inayounganisha barabara kuu na viwanja vya mpira wa miguu (Academic Stadium) yenye urefu wa km 0.69, barabara inayounganisha barabara kuu na Hospital ya Kizimkazi (km0.46), barabara ya Hospital-Sports Stadium (Mgombewa) km 1.72, barabara inayotoka Msikiti wa kihistoria Kizimkazi inayounganisha barabara kuu (km 0.74), barabara ya Hema roundabout- Machomwe (km 2.04), barabara ya Tawi la CCM Dimbani CCM - Kituo cha Kuuza Mafuta (Petrol Station) km 0.34 na barabara inayounganisha barabara kuu na kiwanja cha kufurahishia Watoto (Children sport ground) km 0.6. Mradi huu unatekelezwa na Kampuni ya ECOCITY kwa muda wa miezi mitano kuanzia Disemba 2024. Msimamizi wa mradi huu ni Wakala wa Barabara Zanzibar.

   Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wakala wa Barabara Zanzibar ilipangiwa kutumia jumla ya Shilingi 5,472,320,537 na hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya Shilingi 5,472,320,537 zimepatikana sawa na asilimia 100.

d. **Ujenzi wa Barabara ya Mgelema - Wambaa (km 4.2), Msihakwe - Kipapo - Mgelema (km 0.35) kwa Kiwango cha Lami na Kinyasini-Hospitali ya Wiliaya ya Wete (km 0.7) kwa Kiwango cha Zege.** Wakala wa barabara

ilipanga kuijenga barabara ya Mgelema – Wambaa (km 4.2), kwa kiwango cha lami. Mradi huu pia unajumuisha ujenzi wa barabara ya ndani ya Msihakwe-Kipapo Mgelema jct (km 0.35) kwa kiwango cha lami na barabara ya Kinyasini- Hospitali ya Wilaya ya Wete (km 0.7) kwa kiwango cha lami/zege. Mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi Kampuni ya OCRA na kusimamiwa na Wakala wa Barabara Zanzibar. Mradi utakelezwa kwa muda wa miezi kumi (10) na unatarajia kukamilika ifikapo Septemba, 2025. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025 kazi zilizofanyika ni uwekaji wa tabaka la kwanza la kifusi lenye urefu Kilomita 3.8 barabara ya Mgelema-Wambaa na Kilomita 0.35 tabaka la pili Kiwango cha kifusi barabara ya ndani ya Msihakwe (km 0.35). Hadi Machi 2025, utekelezaji wa kazi za usanifu na ujenzi imefikia asilimia 55.

Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya Shilingi 4,783,900,000. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025 jumla ya Shilingi 2,120,000,000 zimepatikana sawa na asilimia 44.3 ya makadirio ya bajeti.

e. **Ujenzi wa Barabara za Ndani Km 3 Kwa Kiwango cha Kifusi.** Wakala wa Barabara Zanzibar ilipanga kujenga barabara za Mahuduthi-Sipwese (km1), Kirimdomo - Kihogoni (km 0.3), Chwaka ndogo (km 0.7) na Mtamba na Kitondooni (km1) zenye jumla ya urefu wa Kilomita 3 kwa kiwango cha kifusi. Mradi huu unatekelezwa na Wakala wa Barabara Zanzibar na utekelezaji wa kazi za ujenzi kwa kiwango cha kifusi imekamilika kwa asilimia 100.

   Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya Shilingi 193,154,069.00 na hadi kufika Machi, 2025 jumla ya Shilingi 193,154,069.00 zimepatikana sawa na asilima100 ya makadirio ya bajeti.

f. **Matengenezo ya Dharura (Emergence Work) Unguja na Pemba;** Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi,2025 kazi za matengenezo ya dharura zilizofanyika ni ujenzi

wa kalvati iliyokatika maeneo ya Mambosasa Unguja na kwa Pemba ni matengenezo ya dharura ya barabara ya Kichaka – Chwaka (km1.8) kwa kiwango cha kifusi.

Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 jumla ya Shilingi 150,000,000 zilitengwa kwa ajili ya kazi za matengenezo mbalimbali ya dharura na hadi kufika Machi 2025 jumla ya Shilingi 90,000,000 zilipatikana sawa na asilimia 60 ya makadirio.

g. **Matengenezo ya Kawaida ya Barabara (Routine Patchwork);** Wakala wa Barabara ilipanga kuzifanyia matengenezo ya kawaida barabara za Unguja na Pemba zenye urefu wa mita za mraba 8,000 (Unguja mita za mraba 5,000 na Pemba mita za mraba 3,000). Kazi zilizopangwa ni uzibaji wa mashimo kwenye barabara zilizojengwa kwa lami. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 jumla ya mita za mraba 10,068 zilizibwa mashimo, kati hizo, mita za mraba 6,945 ni Unguja na Pemba mita za mraba 3,213 sawa na asilimia 125.9.

Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, jumla ya Shilingi 380,000,000 zilitengwa kwa matengenezo ya kawaida ya barabara (Unguja Shilingi 270,000,000 na Pemba Shilingi 110,000,000) na hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya Shilingi 280,000,000 zilipatikana sawa na asilimilia 73.6 ya makadirio.

h. **Utoaji wa Huduma ya Usimamizi na Ushauri wa Miradi:** Wakala wa Barabara Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imefanikiwa kutekeleza kazi zake za utoaji wa huduma za Usimamizi na Ushauri wa Kitaalamu kwa Wakandasi na wajenzi wa miradi ya barabara Unguja na Pemba. Miradi ya Barabara iliyopatiwa huduma ya usimamizi na ushauri wa kitaalamu ni :- miradi ya ujenzi wa barabara za ndani (km 275.9) Unguja na Pemba zinazofanywa na Kampuni ya IRIS/ARSER JV na MAWI, Ujenzi wa barabara (km12) katika eneo la Bandari mpya ya Mangapwani, Mradi wa Ujenzi wa Barabara Mbalimbali za Ndani na Vijijini (km104) zinazofanywa na Kampuni ya ORKUN Zanzibar Group,

Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kizimbani-Kiboje (Km 7.225) unaotekelezwa na Kampuni ya CCECC pamoja na kusimamia Wakandarasi wote walioingia mikataba ya miradi mbalimbali na Wakala wa Barabara Zanzibar. Aidha Wakala inaendelea na usimamizi wa ujenzi wa mtaro wa maji ya mvua wa soko la Chuini pamoja na barabara ya zege yenye urefu wa mita 400 unaotekelezwa na Mkandarasi EMIRATES Mradi huu utatekelezwa kwa miezi 4 kuanzia mwezi Aprili, 2025.

i. **Uendeshaji wa Shughuli za Ofisi;** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wakala wa Barabara ilipanga kuendelea kuimarisha mazingira ya kazi kwa watumishi wake pamoja na kuwajengea uwezo wafanyakazi 50 kwa kuwaptia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu. Hadi kufikia Machi, 2025 Wakala imefanikiwa kuwajengea uwezo watumishi watatu kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi (Unguja) na watumishi watatu mafunzo muda mrefu (1 Unguja na 2 Pemba). Vilevile, Wakala imefanikiwa kununua vifaa mbalimbali vya ofisi na kusimamia Stahiki za watumishi.

**Matumizi ya Wakala wa Barabara Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.**

**41.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wakala wa Barabara Zanzibar kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 23,723,100,000** ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini kwa ajili ya mishahara, kazi za kawaida na matengenezo ya barabara Unguja na Pemba. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 5,043,900,000** ni mishahara, **Shilingi 679,200,000** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 18,000,000,000** ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

**42.** **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **Shilingi 13,370,040,897** zimetumika sawa na asilimia **56.3** ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,204,477,484** ni mshahara, **Shilingi 167,901,332** ni

matumizi mengineyo na **Shilingi 9,997,662,081** ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara Unguja na Pemba.

## WAKALA WA KARAKANA KUU YA MAGARI ZANZIBAR

43. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Karakana Kuu ya Magari imeanzishwa mwaka 2019 kupitia Tangazo la Serikali la kisheria (Legal Notice No. 136 la Mwaka 2019). Wakala kupitia Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji imepewa jukumu la kuvifanyia matengenezo vyombo vya moto vya Serikali na binafsi kupitia Karakana zake zilizopo Unguja na Pemba pamoja na kutoa ushauri wa ununuzi na uuzaji wa gari za Serikali.

44. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Wakala wa Karakana Kuu ya Magari imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo: -

   a. **Matengenezo ya Vyombo vya Moto (Gari) vya Serikali na Binafsi:** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wakala wa Karakana Kuu ya Magari ilipanga kufanya matengenezo ya vyombo vya moto 2,300 vya Serikali na Binafsi kwa Unguja na Pemba na hadi kufikia Machi, 2025, imefanikiwa kuvifanyia matengenezo vyombo vya moto 1,274 sawa asilimia 55.3 ya makadirio ya mwaka kwa Unguja na Pemba. Kati ya vyombo hivyo, vyombo vya moto 1,206 ni vya Serikali na 68 ni vya watu binafsi. Aidha, jumla ya vyombo 1,093 vimefanyiwa matengenezo Unguja na vyombo 181 vimefanyiwa matengenezo Pemba.

   b. **Utoaji wa Ushauri wa Kitaalamu Juu ya Ununuzi na Uuzaji wa Vyombo vya Moto vya Serikali:** Katika kutekeleza majukumu yake Wakala inaendelea kutoa ushauri wa kitaalam kwa Taasisi za Serikali kabla ya ununuzi wa vyombo vya moto na kuvihakiki baada ya ununuzi. Kwa Mwaka wa Fedha, 2024/2025 Wakala ilipanga kutoa ushauri wa kitaalamu kwa taasisi 40

na hadi kufikia Machi, 2025 Wakala wa Karakana imefanikiwa kutoa ushauri kwa taasisi taasisi 25 sawa na asilimia 62.5. Pia Wakala ilishiriki katika tathmini ya vyombo vilivyonunuliwa na vilivyouzwa na Taasisi hizo ikiwemo OR-TAMISEMIM, ZAFICO, Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na Afisi ya Rais, Fedha na Mipango, ZBC, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ZEMA na Jeshi la Police.

c. **Uimarishaji wa Ofisi na Karakana Unguja na Pemba:** Katika kuimarisha utoaji wa huduma bora za Kiutawala na Kiufundi kwa wakati, Wakala imeimarisha vitendea kazi ikiwemo kuvifanyia matengenezo vyombo vya usafiri, ununuzi wa vifaa vya Ofisi, upatikanaji wa huduma ya mtandao (LAN na INTERNET) na ununuzi wa vipuri. Aidha, Karakana inaendelea kusimamia maslahi ya watumishi wake na kuwapatia stahiki zao kwa wakati ikiwemo mshahara na likizo.

d. **Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi.** Wakala ilipanga kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa wafanyakazi 19 Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi, 2025, imefanikiwa kuwapatia mafunzo wafanyakazi 16 sawa na asilimia 84.2 ya wafanyakazi waliopangiwa kupatiwa mafunzo kwa kipindi hicho. Kati ya wafanyakazi hao, 6 wameapatiwa mafunzo ya muda mrefu (mfanyakazi mmoja Unguja katika ngazi ya Master, wafanyakazi watatu Unguja katika ngazi ya Degree na wafanyakazi wawili katika ngazi ya cheti kwa Unguja mmoja na Pemba mmoja). Aidha wafanyakazi 10 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi kati ya hao, saba Unguja na watatu Pemba.

**Mapato na Matumizi**

45. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wakala wa Karakana Kuu ya Magari ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 1,409,660,000** kupitia vyanzo vyake vya mapato. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025, Wakala ilikadiria kukusanya Jumla ya **Shilingi 1,057,241,400**

na hadi kufikia mwezi wa Machi, 2025, Jumla ya **Shilingi 87,727,138** zilikusanywa sawa na asilimia **8.3** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **6.2** ya makadiri ya mwaka.

46. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wakala wa Karakana Kuu ya Magari ilipanga kutumia Jumla ya **Shilingi 2,875,900,000** ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,981,800,000** ni mshahara na **Shilingi 894,100,000** ni matumizi mengineyo. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi,2025 Wakala wa Karakana Kuu ya Magari ilipanga kutumia Jumla ya **Shilingi 2,191,022,000** kwa kazi za kwaida na Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya **Shilingi 1,358,467,348** zimepatikana sawa na asilimia 62 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 47 ya makadirio ya mwaka kwa Unguja na Pemba. Kati ya fedha, jumla ya **Shilingi 1,062,496,348** ni mshahara na **Shilingi 295,971,000** ni matumizi mengineyo.

47. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ilipangiwa kutumia Jumla ya **Shilingi 1,092,041,074,000** kwa kazi za kawaida na miradi ya maendeleo kwa taasisi zinazosimamia programu hii. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025 ilipangiwa kutumia Jumla ya **Shilingi 784,877,608,004** na hadi kufikia mwezi wa Machi, 2025 jumla ya **Shilingi 460,270,831,822.98** zimetumika sawa na asilimia **58.6** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **42** ya makadirio ya mwaka.

## PP0105 - PROGRAMU YA UJENZI NA MAJENGO.

48. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa usimamizi imara katika kazi za ujenzi na majengo bora ya Serikali na binafsi yaliyo salama na yenye viwango vinavyokubalika kwa mujibu wa miongozo iliyopo na yenye kukidhi mahitaji ya watumiaji wote. Programu hii ina Programu Ndogo moja (1) ambayo ni Programu ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo.

**SP010501 - Programu Ndogo ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo.**

49. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Wakala wa Majengo Zanzibar na ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa usimamizi imara wa ujenzi na majengo bora ya Serikali na binafsi yaliyosalama na yenye viwango vinavyokubalika kwa mujibu wa miongozo iliyopo.

**WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR**

50. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Majengo ina jukumu la kuendeleza majengo ya Serikali, kujenga, kukodisha (Lease or Rent) na kukopesha Majengo ya Serikali kwa bei nafuu kwa watumishi wa umma wanaostahiki, kuandaa na kuweka utaratibu mzuri wa kudhibiti makaazi ya watumishi wa umma, kutoa huduma za Ushauri wa Ujenzi, kusimamia Majengo ya Serikali pamoja na kupanga ujenzi wa Majengo ya Serikali kulingana na mahitaji. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Wakala wa Majengo Zanzibar imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

   a. **Kuandaa Nyaraka za Ujenzi**. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wakala wa Majengo ilipanga kuandaa nyaraka za ujenzi 24 na hadi kufikia Machi, 2024, imefanikiwa kuandaa nyaraka 16 za ujenzi (Ramani na Gharama) sawa na asilimia 67 ya makadirio ya mwaka. Kati ya nyaraka hizo, 10 zimeandaliwa Unguja na 6 zimeandaliwa Pemba. **Kiambatanisho nambari 6A kinahusika**.

   b. **Usimamizi wa Miradi ya Ujenzi.** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wakala wa Majengo ilipanga kusimamia Miradi ya ujenzi 38 na hadi Machi, 2025, imefanikiwa kusimamia miradi ya ujenzi 49 (Construction Supervision) sawa na asilimia 129. Kati ya miradi hiyo 32 imesimamiwa Unguja na 17 imesimamiwa Pemba. **Kiambatanisho nambari 6B kinahusika.**

   c. **Kuandaa Rasimu ya Sheria ya Wakala wa Majengo.** Wakala wa Majengo kwa kushirikiana na Wizara

imefanikiwa kuandaa rasimu ya Sheria ya Wakala wa Majengo ambayo itaiwezesha taasisi hiyo kufanya kazi zake kwa ufanisi. Rasimu hiyo tayari ipo katika hatua za kuwasilishwa kwa Kamati ya Makatibu Wakuu.

**Mapato na Matumizi**

51. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha, 2024/2025, Wakala ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 1,020,500,000** kutoka katika vianzio vyake. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025 Wakala wa Majengo ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 765,375,000** na hadi kufikia Machi, 2025, imefanikiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 468,270,417.44** sawa na na asilimia **61** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **45.8** ya makadirio ya mwaka.

Kwa upande wa matumizi, Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wakala wa Majengo ilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 2,795,300,000** ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 750,000,000** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 2,045,300,000** ni ruzuku ya mshahara. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2025, jumla ya **Shilingi 1,597,110,125** zimetumika sawa na asilimia **57** ya makadirio ya mwaka kwa Unguja na Pemba. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 250,021,093** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 1,347,089,032** ni ruzuku ya mshahara.

**PP0103 - PROGRAMU YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)**

52. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kusimamia uwepo wa miundombinu na huduma bora za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Zanzibar. Matokeo yanayotarajiwa ni kuwepo kwa miundombinu na huduma bora za TEHAMA Zanzibar. Programu hii ina Programu Ndogo moja (1) ambayo ni Programu ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA.

**SP010301 - Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA**.

**53. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara ya Mawasiliano na ina lengo la kuhakikisha na kusimamia kuwepo kwa miundombinu na huduma bora za TEHAMA zilizo salama na endelevu kwa Zanzibar. Vilevile, Idara inasimamia upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya Simu, Posta na Anuani za Makaazi, Mtandao (intaneti) pamoja na kusimamia maendeleo ya huduma za TEHAMA Zanzibar ili kufikia uchumi wa kidijitali.

**54. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Idara ya Mawasiliano ilipanga kuratibu na kusimamia huduma za mawasiliano ya Simu, Intaneti pamoja na huduma za TEHAMA, kuratibu na kusimamia Ujenzi wa Minara katika visiwa vya Unguja na Pemba, kuweka mazingira wezeshi kwa kuimarisha Sekta ya TEHAMA pamoja na kuvutia wawekezaji kwa kuandaa na kuweka Miongozo, Sera, Sheria na Kanuni rafiki (Digital Ecosystem), ili kushajihisha matumizi ya TEHAMA na kuboresha mifumo mbalimbali ya kidijitali, Zanzibar pamoja na kuwajengea uwezo wananchi 4,000 kwa kuwapatia mafunzo ya kutumia mifumo ya kidigitali kupitia vituo vya TEHAMA jamii. Aidha, idara ilipanga kuboresha na kushajihisha matumizi ya mfumo wa Anuani za Makaazi Zanzibar (Engagement with Community).

**55. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Idara ya Mawasiliano imefanikiwa kutekeleza yafauatayo:-

a. **Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano:** Jumla ya Minara 16 ilijengwa Zanzibar katika maeneo ambayo yalionekana kuwa na changamoto ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano. Minara hiyo imejengwa kupitia Makampuni yaliyopatiwa kibali Unguja na Pemba. Orodha ya Makampuni na minara iliyojengwa inaonekana katika **Kiambatanisho nambari 7A**. Ujenzi wa Minara hii ya Mawasiliano ni muendelezo wa juhudi za Serikali katika

kuhakikisha upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano katika maeneo yote ya Zanzibar yanafikia asilimia mia moja. Aidha, Minara ya utoaji wa huduma za mawasiliano ya simu kwa kusafirisha mawimbi kutumia teknolojia ya 2G, 3G, 4G na 5G imeongezeka kutoka 1,545 mwezi Juni 2024 hadi kufikia 1,741 mwezi Machi 2025 sawa na ongezeko la asilimia 12.69. Kuimarika miundombinu ya mawasiliano kumepelekea ongezeko la watumiaji wa huduma hizo ambapo takwimu zinaonesha kuwa, laini za simu zilizosajiliwa Unguja na Pemba zimeongezeka kutoka 896,647 Mwezi Juni, 2024 hadi kufikia laini 1,058, 516 kwa Mwezi Machi, 2025 sawa na ongezeko la asilimia 18.05. **Kiambatanisho nambari 7B na 7C vinatoa ufafanuzi.**

b. **Ukaguzi wa Upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano:** Idara ya Mawasiliano kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) zinaendelea na ukaguzi na uchambuzi wa upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano katika maeneo ya visiwa vidogo vidogo 48 hapa Zanzibar. Visiwa hivyo pia vimetambuliwa kama maeneo muhimu yanayohitaji ufuatiliaji wa karibu wa huduma za mawasiliano ili kuendana na Sera ya Mageuzi ya kidijitali pamoja na Sera ya Uchumi wa Buluu, kwa lengo la kuvutia uwekezaji, kuongeza ulinzi wa nchi na kuwezesha shughuli za kitalii kwenye visiwa vinavyotumika kwa utalii. Hali ya upatikanaji wa mawasiliano katika visiwa vidogo vidogo imeanishwa katika **Kiambatanisho nambari 7D** ambapo mawasiliano katika visiwa vyote yanapatikana.

c. **Utoaji Mafunzo ya TEHAMA kupitia Vituo vya TEHAMA Jamii:** Idara ya Mawasiliano kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025 ilipanga kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa wananchi 4000, ambapo hadi Machi 2025, Idara imefanikiwa kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa wanajamii wapato 1,524 sawa na asilimia 38.1. Kati yao, wanawake ni 950 na wanaume ni 574. Mafunzo hayo yanajumuisha

program  kuu mbili (2) ambazo ni mafunzo ya usalama wa mtandao na TEHAMA kwa Jamii. Jumla ya vijana 404 wamepata mafunzo ya usalama wa mtandao. Kati yao 219 ni wanawake na 185 ni wanaume. Kwa upande wa mafunzo ya TEHAMA kwa Jamii, jumla ya wananchi 1,120 wamepatiwa mafunzo hayo, kati yao 731 ni wanawake na 389 ni wanaume. Lengo la mafunzo haya ni kupunguza idadi ya wanajamii wasiojua kutumia Kompyuta na mitandao ili waweze kushiriki katika uchumi wa kidijitali.

d. **Kuweka Mazingira Wezeshi kwa Kuimarisha Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:** Idara ya Mawasiliano imeifanyia mapitio Sera ya TEHAMA ya mwaka 2013 na kuamua kuandaa rasimu ya Sera mpya ya Mageuzi ya Kidijitali Zanzibar 2025 (Zanzibar Digital Transformation Policy 2025) ambapo ipo katika hatua za mwisho za kuiwasilisha rasimu ya Sera hiyo Serikalini. Vilevile, Idara imetunga rasimu ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Faragha, Sheria ambayo ni takwa la Kikanda (Afrika Mashariki) na Kimataifa (International) ili kuweza kulinda taarifa hizo kwa misingi ya Sheria pamoja na kuvutia wawekezaji.

e. **Kusimamia na Kuratibu Matumizi ya Anuani za Makaazi:** Mfumo wa Anwani za Makazi ni miundombinu inayotambulisha mahali halisi ambapo kitu, mtu au huduma inapopatikana pamoja na kuwezesha urahisi wa ufikiwaji wake, sambamba na kuwezesha biashara mtandao (e-Commerce). Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara kupitia Idara ya Mawasiliano kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (SMT),  Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa  na Idara Maalum za SMZ, imeanzisha huduma ya utoaji wa barua za utambulisho wa mwananchi kutoka kwa Sheha kwa njia ya kidijitali. Wananchi wanaomba huduma hiyo bila kufika katika ofisi za Shehia kwa kutumia Mfumo wa Kidijitali wa Anuani za Makaazi

(NaPA). Kwa sasa huduma hii inafanywa kwa majaribio katika Shehia za Kizimkazi-Dimbani na Gulioni kwa Unguja pamoja na Shehia za Konde na Kinowe kwa Pemba. Hadi kufikia Machi 2025 jumla ya barua 230 zimetolewa kwa njia ya kidijitali katika Shehia hizo.

Katika kufanikisha kazi hii jumla ya watendaji 46 wamepewa mafunzo ya utekelezaji wa kazi hiyo Unguja na Pemba. Watendaji hao wanatoka katika Halmashauri, Mabaraza ya Miji, Manispaa, Masheha na Makatibu wa Masheha. Aidha, watendaji wa Shehia za Gulioni, Kizimkazi-Dimbani, Konde na Kinowe wamepewa Kompyuta, Printa na Vishkwambi kwa ajili ya kufanikisha kazi hizo. Katika kipindi hicho zoezi la uhakiki wa Anuani za Makaazi liliendelea katika Wilaya za Mkoani na Wete ambapo jumla ya Anuani za Makaazi 33,358 zimehakikiwa na jumla ya nyumba na majengo 4,828 zimewekewa Anuani za Makaazi.

56. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Programu hii ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA ilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 6,687,907,000** kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 287,207,000** ni mshahara, **Shilingi 400,000,000** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 6,000,000,000** ni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **Shilingi 2,475,961,375** zimetumika sawa na asilimia 37 ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo **Shilingi 228,038,717** ni mshahara, **Shilingi 50,060,000** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 2,197,862,658** ni kwa ajili ya kazi za maendeleo.

## PP0104 - UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI

57. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwa Wizara inaratibu na kutayarisha Sera na Mipango bora katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji pamoja na usimamizi mzuri wa rasilimali watu. Programu hii ina

programu ndogo tatu (3) ambazo ni:- Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti pamoja na Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba.

### SP010401 - Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji

58. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi na ina lengo la kuimarisha huduma za ofisi na usimamizi wa rasilimali watu. Utekelezaji wa programu hii ndogo ni kama ifuatavyo: -

### IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

59. **Mheshimiwa Spika,** Idara hii imepewa jukumu la kusimamia na kutathmini shughuli za uendeshaji wa Wizara na kushughulikia maslahi pamoja na nidhamu kwa wafanyakazi. Aidha, Idara inaandaa na kusimamia mpango wa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wafanyakazi wa Wizara pamoja na utunzaji wa kumbukumbu na mali za Wizara. Pia, Idara inajukumu la kuimarisha mazingira mazuri ya utendaji kazi kwa kuhakikisha vitendea kazi vinapatikana kwa wakati. Vilevile, Idara inatoa huduma za ununuzi na usimamizi wa mapato na matumizi ya Wizara.

60. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Idara ya Uendeshaji na Utumishi kupitia Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji ilipanga kuwajengea uwezo wafanyakazi hamsini (50) wa Wizara Unguja na Pemba kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ili waweze kutoa huduma bora na kwa ufanisi. Aidha, Idara ilipanga kuimarisha huduma za kiutawala na utumishi ikiwemo kuweka mazingira mazuri ya kazi, kusimamia maslahi ya watumishi pamoja na kuongeza vitendea kazi kwa lengo la kuleta ufanisi. Vilevile, Idara ilipanga kutoa Makala na machapisho mbalimbali kuhusu utekelezaji wa shughuli na mafanikio ya Wizara pamoja na kuufanyia mapitio Mkataba wa Huduma kwa Umma.

61. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imefanikiwa kuwapatia mafunzo mbalimbali wafanyakazi hamsini na mbili (52) Unguja na Pemba sawa na asilimia 104 ya wafanyakazi waliopangwa kupatiwa mafunzo hayo. Kati ya hao, wafanyakazi kumi na nane (18) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi tofauti katika Vyuo vya ndani na Nje ya nchi na wafanyakazi thelathini na nne (34) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika kozi tofauti. **Kiambatanisho nambari 8A na 8B kinahusika**.

62. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha mazingira mazuri ya kazi kwa watendaji yanaimarika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imefanya ukarabati wa majengo ya Ofisi, imevifanyia matengenezo vyombo vya usafiri vya Wizara, kuwapatia vitendea kazi kwa kununua vifaa mbalimbali vya Ofisi pamoja na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao kwa wakati ikiwemo malipo ya mishahara, malipo ya likizo pamoja na malipo baada ya saa za kazi. Aidha, Idara imefanikiwa kuufanyia mapitio Mkataba wa Huduma kwa Umma na kutayarisha Mkataba mpya ambao utatumika kwa muda wa miaka mitatu ijayo 2025 - 2028.

63. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Idara ya Uendeshaji na Utumishi kupitia Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji ilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 3,376,262,000** kwa kazi za kawaida, ikiwa **Shilingi 1,822,862,000** ni mshahara na **Shilingi 1,553,400,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **Shilingi 1,601,550,179.5** zimetumika sawa na asilimia **47.4** ya makadirio ya Bajeti. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,171,305,229.5** ni Mshahara na **Shilingi 430,244,950** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

### SP010402 - Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara

64. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara ya

Mipango, Sera na Utafiti na ina lengo la kuhakikisha Mipango na Sera za Wizara zinatekelezwa.

**IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

**65.** **Mheshimiwa Spika,** Idara hii imepewa jukumu la kupanga, kuratibu, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa Sera na Mipango ya Sekta za Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Aidha, Idara inaratibu kazi zote za maendeleo ya Wizara ikiwemo kubuni, kutayarisha na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Pia, Idara inajukumu la kubuni na kufanya tafiti za kisekta ikiwemo ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu.

**66.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ilipanga kuendelea kuratibu na kufuatilia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kutayarisha Muongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara, kutoa mafunzo ya utayarishaji wa bajeti kwa watendaji, kuratibu na kufanya tafiti zinazohusu Sekta za Wizara, kukamilisha Sera ya mageuzi ya Kidigital itakayosimamia masuala ya TEHAMA. Vilevile, Idara ilipanga kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo pamoja na kukusanya takwimu mbalimbali katika sekta zinazosimamiwa na Wizara.

**67.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

a. Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanikiwa kufuatilia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikishirikiana na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ikiwemo miradi ya ujenzi wa barabara, miundombinu ya Viwanja vya Ndege na Bandari.

b. Idara inaendelea kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayosimamiwa na Wizara,

kutayarisha ripoti mbalimbali za utekelezaji wa kazi za Wizara pamoja na kukusanya takwimu zinazohusu sekta zinazosimamiwa na Wizara.

c. Idara ya Mipango ikishirikiana na Idara ya Mawasiliano imekamilisha kutayarisha Rasimu ya Sera ya Mageuzi ya Kidijital itakayosimamia masuala ya TEHAMA. Hatua inayoendelea kwa sasa ni kuwasilishwa kwa Kamati ya Makatibu Wakuu ili kupata maoni yao na hatimae kuwasilishwa katika kikao cha Baraza la Mapinduzi kwa maamuzi.

d. Idara imefanikiwa kuratibu shughuli mbalimbali zinazohusu Sekta ya Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano ikiwemo kushiriki mikutano mbalimbali inayajadili maendeleo ya Sekta hizo.

e. Idara imefanikiwa kutoa mafunzo ya utayarishaji wa Bajeti kwa wafanyakazi wa Wizara kutoka Idara na Taasisi tofauti. Mafunzo hayo yalitolewa kwa kushirikiana na Idara ya Bajeti kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar.

f. Idara imefanikiwa kuendelea kuratibu Taasisi na Mashirika mbalimbali yanayojitegemea yaliyo chini ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na kuratibu na kushiriki katika vikao vya Mashirikiano baina ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na uchukuzi Zanzibar na Wizara ya Ujenzi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo kuimarisha mashirikiano pamoja na kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta ya Ujenzi.

g. Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inaendelea kutayarisha Sheria mbalimbali za Sekta ya Ujenzi, Usafiri na Mawasiliano ikiwemo Sheria ya uanzishwaji wa Wakala wa Majengo, Sheria ya Karakana, Sheria ya Wakala wa Barabara pamoja na Marekebisho ya Sheria Namba 5 ya Usafiri wa Baharini ya Mwaka 2006. Sheria zote hizi ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

68. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 886,739,000** kwa kazi za kawaida, ikiwa **Shilingi 352,439,000** ni mshahara na **Shilingi 534,300,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **Shilingi 406,899,105** zimetumika sawa na asilimia **45.8** ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 322,899,105** ni mshahara na **Shilingi 84,000,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**SP010403 - Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba.**

69. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Ofisi Kuu – Pemba yenye lengo la kuhakikisha majukumu ya Wizara kwa upande wa Pemba yanatekelezwa ipasavyo.

**OFISI KUU – PEMBA**

70. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu – Pemba kupitia Program ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba imepewa jukumu la kuratibu na kusimamia kazi zote za Wizara kwa upande wa Pemba. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Ofisi Kuu Pemba imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

a. Imeratibu na kusimamia maslahi ya wafanyakazi pamoja na kutoa huduma mbali mbali za Ofisi kwa lengo la kuweka mazingira bora ya kiutendaji. Huduma zilizotolewa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya Ofisi, malipo ya likizo kwa watumishi, malipo baada ya saa za kazi, malipo ya safari kikazi, kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi pamoja na mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi, kulipia huduma za uendeshaji wa Ofisi pamoja na kufanya matengenezo madogo madogo ya Jengo la Ofisi lililopo Tibirinzi Chake Chake Pemba.

b. Ofisi kuu Pemba imefanikiwa kuratibu na kusimamia utaoji wa mafunzo ya TEHAMA kupitia Vituo vya

TEHAMA jamii kwa Wilaya zote za Pemba, kuratibu zoezi la kuendeleza Anuani za Makaazi kwa kufanya uhakiki pamoja na usajili mpya wa makaazi ambayo hayakusajiliwa katika hatua za awali kwa Wilaya za Mkoani na Wete pamoja na kuratibu maboresho ya Mfumo wa Anuani za Makaazi kwa kuazisha barua ya utambulisho itakayokua na uwezo wa kuhifadhi taarifa za wananchi na ambayo itakua inatumika kuanzia ngazi ya shehia.

c. Ofisi Kuu Pemba imefanikiwa kusimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi ya Ujenzi wa Miundombinu ya Barabara, Uwanja wa Ndege wa Pemba pamoja na Bandari za Mkoani na Shumba inayetekelezwa kwa upande wa Pemba.

**71.** **Mheshimiwa Spika** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi Kuu Pemba kupitia programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba ilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 1,262,492,000** kwa kazi za kawaida, ikiwa **Shilingi 762,492,000** ni mshahara na **Shilingi 500,000,000** ni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **Shilingi. 574,334,663** zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia **45.4** ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha **hizo, Shilingi 402,334,663** ni mshahara na **Shilingi. 172,000,000** ni matumizi mengineyo.

**72.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mapato, Ofisi Kuu Pemba kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 791,840,000.** Ikiwa **Shilingi 290,340,000** zilikadiriwa kukusanywa kupitia Wakala wa Karakana Kuu ya Magari na **Shilingi 501,500,000** zilikadiriwa kupitia Wakala wa Majengo. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2024/2025 Ofisi Kuu Pemba ilikadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 593,873,700**. Ikiwa **Shilingi 217,748,700** kupitia Wakala wa Karakana Kuu ya Magari na **Shilingi 376,125,000** kupitia Wakala wa Majengo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2025 Ofisi Kuu imefanikiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 116,717,756** sawa na asilimia **19.65** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **14.74** ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha

hizo, **Shilingi 7,116,000** zilikusanywa kupitia Wakala wa Karakana ya Magari na **Shilingi 109,601,756** zilikusanywa kupitia Wakala wa Majengo.

## E. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA MALENGO YA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA KIBAJETI ZILIZO CHINI YA WIZARA.

**73. Mheshimiwa Spika,** Kama nilivyoeleza hapo awali kuwa, Wizara ina Taasisi kumi na moja (11) zinazojitegemea. Kati ya Taasisi hizo,Taasisi tatu (3) hazijitegemei kibajeti na zinapata ruzuku kutoka Serikalini, Taasisi hizo ni Wakala wa Barabara, Wakala wa Majengo na Wakala wa Karakana Kuu ya Magari. Maelezo ya utekelezaji wa Taasisi hizi pamoja na malengo yake yameelezwa kwenye Programu za Wizara.

**74. Mheshimiwa Spika,** Taasisi nane (8) zilizosalia, kati ya Taasisi kumi na moja (11) zinazojitegemea kibajeti kupitia mapato wanayokusanya na matumizi yake huidhinishwa na Bodi za Taasisi husika. Taasisi hizo ni:- Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani, Mamlaka ya Usafiri Baharini, Shirika la Bandari, Shirika la Meli, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi, Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo na Shirika la Mawasiliano (ZICTIA). Utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 na malengo yanayotarajiwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni kama ifuatavyo:-

### E.1. MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI ZANZIBAR

**75. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ina jukumu la kusimamia usafiri barabarani kwa kudhibiti usalama wa watumiaji wa barabara, utoaji wa huduma za usafiri barabarani pamoja na kusimamia Kamati ya Kitaifa ya Usalama Barabarani. Aidha, katika kutekeleza majukumu hayo kwa mujibu wa Sheria nambari 7 ya mwaka 2003, Sheria ya Usafiri Barabarani, Mamlaka inafanya shughuli za ukaguzi wa vyombo vya moto na kutoa leseni za njia kwa vyombo hivyo (Road license), kutoa leseni kwa

vyuo vya udereva na walimu wao, kutoa leseni za madereva wanafunzi (learner), kuwafanyia majaribio ya nadharia na vitendo madereva wanafunzi, kutoa ruhusa za njia na usafirishaji wa abiria na mizigo, kutoa leseni za vyombo vya biashara, kutoa beji za utingo na madereva pamoja na kutoa vibali na kubadilisha leseni kwa madereva wa kigeni wanaotaka kuendesha vyombo vya moto hapa Zanzibar.

**Utekelezaji wa Malengo ya Mamlaka kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.**

**76. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani imetekeleza kazi zifuatazo: -

a. **Ukaguzi wa Vyombo vya Moto:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilipanga kufanya ukaguzi wa vyombo vya moto 76,629 na kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 ilipanga kukagua vyombo 57,472 kwa Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi 2025 jumla ya vyombo vya moto 35,639 vimekaguliwa sawa na asilimia 62 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 47 ya mwaka. Kati ya vyombo hivyo 30,075 vimekaguliwa Unguja na 5,564 vimekaguliwa Pemba. **Kiambatanisho namba 9 A kinahusika.**

b. **Utoaji wa Ruhusa za Njia na Usafirishaji:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilipanga kutoa ruhusa za njia na usafirishaji 22,363 na kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025 ilipanga kutoa ruhusa za njia 16,772. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya ruhusa za njia na usafirishaji 14,435 kwa gari mbalimbali zinazotoa huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo zimetolewa Unguja na Pemba sawa na asilimia 86 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 65 ya makadirio ya mwaka. Kati ya ruhusa hizo, 13,125 zimetolewa Unguja na ruhusa 1,310 zimetolewa Pemba. **Kiambatanisho namba 9B kinahusika**.

c. **Utoaji wa Leseni kwa Gari za Biashara:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilipanga kutoa leseni 15,762 kwa gari za biashara na kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 imepanga kutoa leseni 11,822 kwa Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya leseni 15,565 za usafirishaji zimetolewa kwa gari za biashara aina mbalimbali zinazotoa huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo sawa na asilimia 132 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 99 ya makadirio ya mwaka. Kati ya leseni hizo, leseni 14,931 zimetolewa Unguja na leseni 634 zimetolewa Pemba.

d. **Majaribio ya Madereva:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilipanga kuwafanyia majaribio ya nadharia na vitendo madereva wanafunzi 14,436 na kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 ilipanga kuwafanyia majaribio madereva 10,827 Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi, 2025, Mamlaka imefanikiwa kuwafanyia majaribio ya nadharia na vitendo jumla ya madereva wanafunzi 23,912 sawa na asilimia 221 ya makadirio ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 166 ya makadirio ya mwaka. Ikiwa madereva 21,401 wamefanyiwa Unguja na madereva 2,511 wamefanyiwa Pemba.

e. **Utoaji wa Beji za Utingo na Madereva:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilipanga kutoa beji za utingo na madereva wa vyombo vya biashara aina mbalimbali 12,644 na kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 ilipanga kutoa beji za utingo na madereva wa vyombo vya moto 9,483 Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya beji 7,586 zimetolewa kwa utingo na madereva wa vyombo vya moto aina mbali mbali sawa na asilimia 80 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 60 ya makadirio ya mwaka. Kati ya beji hizo 6,463 zimetolewa Unguja na 1,123 zimetolewa Pemba. Kiambatanisho namba 9 C kinahusika.

f. **Utoaji wa Leseni za Madereva Wanafunzi (Learner Licences):** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilipanga kutoa leseni za kujifundishia vyombo vya moto kwa madereva wanafunzi 24,336 na kwa kipindi cha miezi tisa ilipanga kutoa leseni 18,252 Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya leseni za madereva wanafunzi 16,563 zimetolewa sawa na asilimia 91 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 68 ya makadirio ya mwaka. Kati ya leseni hizo, 14,068 zimetolewa Unguja na 2,495 zimetolewa Pemba.

g. **Utoaji wa Vibali Kwa Madereva Wageni:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilipanga kutoa vibali 28,363 na kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 ilipanga kutoa vibali 21,272 kwa madereva wageni. Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya vibali 19,670 vya ruhusa ya kuendesha vyombo vya moto kwa wageni vimetolewa Unguja na Pemba sawa na asilimia 92 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 69 ya makadirio ya mwaka.

**Utekelezaji wa Miradi ya Mamlaka**

77. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani imetekeleza miradi ifuatayo: -

a. **Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Vyombo vya Moto:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilipanga kujenga Kituo cha Kisasa cha Ukaguzi wa Vyombo vya Moto katika eneo ya Dole. Hadi kufikia Machi, 2025 mradi huu umekamilika kwa asilimia 100 na Kituo hicho kimeanza kufanya kazi rasmi tarehe 17 Machi, 2025.

b. **Mradi wa ZIMS - ZARTSA Integrated Management System:** Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2024/2025 iliendelea na kutekeleza mradi wa Mfumo Mkuu wa Mamlaka ambao unajumuisha Moduli zote za utoaji wa huduma za usafiri na usalama barabarani Zanzibar.

Jumla ya moduli nane (8) zimekamilika katika mfumo huo na Mamlaka kwa sasa iko katika hatua za mwisho za kuwapa mafunzo wafanyakazi pamoja na wadau wengine wa Sekta ya Usafiri ili kuweza kuufanyia kazi.

**Mapato na Matumizi**

**78.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 5,508,018,510** Unguja na Pemba na kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Mamlaka ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 4,131,012,884** na hadi kufikia Machi 2025, jumla ya **Shilingi 4,380,996,228** zimekusanywa sawa na asilimia **106** ya makadirio ya miezi tisa sawa na asilimia **80** ya makadirio ya mwaka.

**79.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ilipanga kutumia jumla ya **Shilingi 5,508,018,510** ikiwa **Shilingi 2,164,517,964** ni mshahara, **Shilingi 1,343,500,546** kazi za kawaida na **Shilingi 2,000,000,000** ni mchango wa Mamlaka kwa Serikali kuu.

Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Mamlaka ilipanga kutumia **TSH 4,131,012,884**. Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **Shilingi 3,496,157,149** zimetumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida na mshahara sawa na asilimia **63** ya makadirio ya mwaka na asilimia **85** ya makadirio ya miezi tisa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,219,752,500** ni mshahara na **Shilingi 952,404,651** ni matumizi ya kawaida. Aidha, katika kipindi hicho Jumla ya **Shilingi 1,323,999,998** zimewasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ikiwa ni mchango wa Mamlaka kwenda Serikali Kuu.

**MALENGO YA MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI YANAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.**

**80.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar imepanga kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuendelea kutoa huduma za usafiri barabarani zenye ufanisi kwa Unguja na Pemba zikiwemo: Utoaji wa leseni za madereva wanafunzi 26,051, Kuvifanyia ukaguzi vyombo vya moto 76,626, Kuwafanyia majaribio ya udereva madereva 16,256, Kutoa vibali kwa madereva wageni 35,217, Kutoa leseni kwa vyombo vya Biashara 23,198, Kutoa ruhusa za njia za usafirishaji 24,406 na Kutoa beji za madereva na utingo 11,949.

ii. Kuendelea kutekeleza mradi wa mageuzi ya utoaji wa huduma kwa njia ya mifumo (ZIMS- ZARTSA Intergrated Management System) ambapo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Mamlaka itaendelea na matumizi ya mfumo huo kwa utoaji wa huduma zake.

iii. Kuufanyia marekebisho Mfumo wa Adhabu za Papo kwa Papo kwa kuweka Kamera za Kisasa za Usalama Barabarani ili kuweza kuwabaini madereva wa vyombo vya moto wanaofanya makosa barabarani.

iv. Kuendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Ajali Barabarani ili kuimarisha usalama wa watumiaji wa barabara kwa kuwapatia elimu ya usalama barabarani makundi tofauti ya jamii pamoja na kufanya ukaguzi wa barabarani ili kubaini wanaokiuka utaratibu.

v. Kujenga kituo cha Upasishaji Madereva Zanzibar pamoja na kuanzisha Mfumo wa Udhibiti wa Usalama Barabarani (Traffic Managemnt System) ambao utahusisha uandaaji wa Mfumo wa Usajili wa Vyombo utakaoendana na mifumo ya Mamlaka ikiwemo Mfumo wa Vifaa vya Kufuatilia Vyombo vya Moto (Vehicles Tracking System) na Mfumo wa "taxi" Mtandao.

**Makadirio ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**81. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani imekadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 6,177,981,800** kupitia vyanzo vyake mbalimbali na imepanga kutumia jumla ya **Shilingi 6,177,981,800** kwa

kazi za kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,073,794,864** ni mshahara, **Shilingi 2,104,186,936** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 2,000,000,000** ni mchango wa Mamlaka kwa Serikali Kuu.

## E.2. MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR

**82. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka Usafiri Baharini, kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri Baharini Nambari 5 ya Mwaka 2006 na Sheria ya Mamlaka ya Usafiri Baharini nambari 3 ya Mwaka 2009, ina jukumu la kusimamia, kudhibiti na kuendeleza Sekta ya Usafiri wa Baharini. Miongoni mwa kazi zake ni: Usajili wa Meli, Usimamizi na Udhibiti wa Ulinzi na Usalama wa Meli na Bandari, Usimamizi wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari yatokanayo na Meli, Utoaji wa leseni kwa Vyombo Vidogo Vidogo vya Baharini, Ukaguzi wa Meli na Vyombo Vidogo Vidogo, Uchunguzi wa ajali za Baharini, Usimamizi na Udhibiti wa huduma za Bandari na Meli, Usimamizi wa Ustawi na maslahi ya Mabaharia, Uratibu wa Utafutaji na Uokozi Baharini, Ukaguzi wa Meli za Kigeni zinapokuwa katika Bandari za Zanzibar, Utoaji wa Vyeti, Leseni, Vibali, Vitambulisho pamoja na Vitabu vya Kumbukumbu za Mabaharia.

**Utekelezaji wa Kazi za Mamlaka kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**.

**83. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Mamlaka ya Usafiri Baharini imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo: -

a. **Usajili wa Meli za Kimataifa na Meli za Ndani**. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025 Mamlaka ilikadiria kusajili jumla ya Meli 256, hadi kufikia mwezi wa Machi, 2025 jumla ya Meli 292 zilisajiliwa zenye uzito GT 2,133,946 sawa na asilimia 114 ya makadirio. Kati ya hizo, Meli 276 kwa usajili wa Meli za Kimataifa zenye GT 2,105,393 na Meli 16 kwa usajili wa ndani zenye GT 26,553. Ongezeko hilo linatokana na Mamlaka kuendelea kuyafanyia kazi kwa wakati mara maombi ya usajili yanapofika, kuongezeka kwa wakaguzi ambao hufanya

ukaguzi wa meli hizo kabla ya usajili pamoja na kufanya kazi kwa ukaribu na Taasisi zinazojishughulisha na usimamizi wa meli.

b. **Usajili wa Vyombo Vidogo Vidogo na Leseni za Mabaharia:** Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 Mamlaka ilipanga kusajili jumla ya vyombo Vidogo Vidogo 1,125 ambapo hadi kufikia Machi, 2025, Mamlaka ilisajili vyombo vidogo vidogo 1,451 sawa na asilimia 128 ya makadirio. Aidha, Mamlaka ilikadiria kutoa leseni 900 hadi kufikia Machi 2025, Mamlaka imefanikiwa kutoa leseni 1,026 za manahodha waliofaulu mitihani na kupewa vyeti vya unahodha sawa na asilimia 114 ya makadirio. Ongezeko hilo linatokana na Mamlaka kusogeza huduma zake karibu na wananchi kwa kuweka mfumo wa Usajili wa vyombo hivyo katika ofisi zake za Mkokotoni na Pemba, kuweka ofisi ndogo katika Mkoa wa Kusini Unguja, Kufanya doria na kutoa elimu mara kwa mara kwa watumiaji na wamiliki wa vyombo hivyo juu ya umuhimu wa usajli na usalama wa vyombo vyao.

c. **Kuthibitisha Vyeti vya Mabaharia wa Kigeni:** Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025 Mamlaka ilipanga kuthibitisha vyeti 960 vya Mabaharia vya ngazi ya maofisa wanaofanya kazi katika Meli za Kimataifa (TZIRS) zilizochini ya Usajili wa Mamlaka na kuthibitishwa (endorsement) Vyeti vya umahiri (Certificate of Competency). Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya Mabaharia 1,111 wamethibitishwa (Endorsement) vyeti vyao vya umahiri (Certificate of Competency) sawa na asilimia 116 ya makadirio. Ongezeko hilo linatokana na usajili wa Meli mpya ambazo huajiri maofisa wapya.

d. **Vitabu vya Mabaharia (Discharge Book):** Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025 Mamlaka ilipanga kutoa vitabu vya mabaharia 1,500 hadi kufikia Machi 2025, jumla ya mabaharia 518 wamepewa vitabu sawa na asilimia 35 ya makadirio.

e. **Kuthibitisha Vyeti na Mikataba ya Mabaharia Wanaosafiri Nje ya Nchi.** Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Mamlaka ilipanga kuthibitisha vyeti 480 ambapo hadi kufikia Machi 2025, Mamlaka imeweza kuthibitisha vyeti 146 sawa na asilimia 30.4 ya makadirio. Aidha, Mamlaka ilipanga kuthibitisha Mikataba 500 ya Mabaharia wanaosafiri na Meli za nje kupitia Kampuni ya DANAOS na hadi kufikia Machi, 2025, Mamlaka ilithibitisha Mikataba 1,018 sawa na asilimia 203.6 ya makadirio. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa meli katika Kampuni ya DANAOS, kwa kutanua biashara na kununua meli za Bulk Carrier ambapo awali walikua na meli za Kontena tu.

f. **Utoaji leseni kwa Kampuni na Taasisi mbali mbali zinazotoa Huduma Bandarini na Melini.** Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025 Mamlaka ilikadiria kutoa leseni 377 kwa Taasisi zinazotoa huduma za usafiri baharini. Hadi kufikia Machi, 2025, Mamlaka imefanikiwa kutoa Leseni 163 kwa taasisi hizo, ikiwa ni sawa na asilimia 43.2 ya makadirio. Miongoni mwa huduma ziliotolewa ni: - Watoaji Mizigo Bandarini (Clearing and Forwarding), “Diving Center”, “Water Sport”, Kampuni yenye Meli moja na Kampuni zenye meli zaidi ya moja, Wakala wa Kuuza Ticket (Ship Representantives).

g. **Ukaguzi wa Meli**. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025, Mamlaka ilipanga kukagua jumla ya Meli 89 za ndani na hadi kufikia Machi 2025, jumla ya Meli 57 sawa na asilimia 64 ya makadirio zimekaguliwa. Kati ya Meli hizo, Meli 14 zilifanyiwa ukaguzi wa awali, Meli 27 zilifanyiwa ukaguzi wa kiusalama wa mwaka, Meli 5 zilifanyiwa ukaguzi wa chelezoni na Meli 11 zilifanyiwa ukaguzi wa kushtukiza zenye jumla ya GT 58,780.

h. **Huduma kwa Abiria Wanaosafiri Kupitia Vyombo vya Baharini.** Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Mamlaka ilikadiria kuhudumia abiria 1,810,450

wanaosafiri kupitia Bandari za Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya abiria 1,542,643 walisafiri sawa na asilimia 85 ya makadirio kupitia bandari za Unguja na Pemba.

i. **Kutayarisha Miongozo na Kanuni za Mamlaka:** Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Mamlaka ya Usafiri Baharini imepanga kutayarisha jumla ya Kanuni 3 na Miongozo 20 kwa ajili ya kufanyia kazi. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2024 Mamlaka ilitayarisha Kanuni 1 sawa na asilimia 33 na Miongozo 14 sawa na asilimia 70 ya makadirio.

j. **Kuwajengea Uwezo Wafanyakazi wa Mamlaka:** Katika kipindi cha Julai, 2024, hadi Machi 2025, Mamlaka imeweza kuwajengea uwezo wafanyakazi 58 kwa kuwapatia mafunzo katika fani mbali mbali ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Kati ya hao, wafanyakazi 18 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi yanayohusu ukaguzi wa Meli, uthibitishaji wa vyeti vya mabaharia (re–validation) usimamizi wa bandari, wafanyakazi 9 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu, wafanyakazi 27 walipatiwa Mafunzo ya Uongozi Mkakati (Strategic Leadership), mfanyakazi 1 mafunzo ya Mpango Mkakati (Strategic Planning) na wafanyakazi 2 mafunzo ya kujiandaa na kustaafu kazi na mfanyakazi 1 mafunzo yanayohusiana na uandishi wa Sheria.

k. **Uboreshaji wa Huduma za Mamlaka:** Mamlaka imesogeza huduma zake karibu na wananchi na kuweka mfumo wa Usajili wa vyombo vidogo vidogo katika ofisi zake za Mkokotoni na Pemba, hali hii imeongeza wigo wa vyombo ambavyo vimesajiliwa na kuwapunguzia shida Wananchi pale ambapo wanahitaji kusajili vyombo vyao na kupelekea kuongezeka mapato ya Mamlaka.

l. **Kufungua Ofisi za Mamlaka katika Mkoa wa Kusini Unguja:** Mamlaka imeweza kuweka ofisi yake katika ofisi ya Mkoa wa Kusini Unguja na Kufanya doria na

kutoa elimu mara kwa mara kwa watumiaji na wamiliki wa vyombo hivyo vidogo vidogo, juu ya umuhimu wa Usajli na Usalama wa vyombo vyao. Hali hii imepelekea ongezeko la uelewa juu ya huduma za Mamlaka na watumiaji wa Bahari kuwa na elimu juu ya kuchukua tahadhari na kujilinda na majanga mbali mbali ambayo yanaweza kutokea Baharini.

m. **Kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Hazina:** Mamlaka imefanikiwa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Hazina jumla Shilingi 1,668,750,003. Hii inatokana na kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali na usimamizi mzuri wa matumizi ya kazi za Mamlaka.

**Mapato na Matumizi**

**84. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 7,938,815,140** kupitia vyanzo vyake vya mapato. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 Mamlaka ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 5,943,281,503** na hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **Shilingi 6,032,020,647** zimekusanywa sawa na asilimia **101** ya makadirio ya robo tatu na asilimia **70** kwa makadirio ya mwaka.

Kwa upande wa matumizi, Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, ilikadiria kutumia jumla ya **Shilingi 7,428,993,487** kwa kazi za kawaida, Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025, ilipanga kutumia **Shilingi 5,430,412,027** na hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **Shilingi 4,505,086,631** zimetumika sawa na asilimia **83** ya makadirio ya robo tatu na asilimia **61** kwa makadirio ya bajeti ya mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,598,647,480.9** ni mshahara, **Shilingi 1,237,689,146.7** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 1,668,750,003** zimeingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ikiwa ni Mchango wa ZMA.

**MALENGO YA MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.**

**85. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imepanga kutekeleza yafuatayo: -

i. Mamlaka imepanga kusajili jumla ya Meli 16 za ndani na 240 za kimataifa, kutoa jumla ya leseni 1,500 kwa vyombo vidogo vidogo, vitabu 1,800 vya Mabaharia (Discharge Books), kuthibitisha Mikataba 960 ya Mabaharia, kuthibitisha Vyeti 192 vya mafunzo ya Ulinzi Melini (Maritime Security awareness) kwa Mabaharia wanaosafiri na Meli za nje kupitia Kampuni ya DANAOS, kutoa vitambulisho vya Mabaharia (Seafares ID) 600 na kuthibitisha Vyeti 600 vya Mabaharia wa Kigeni (Endorsements).

ii. Vile vile, Mamlaka imepanga kutoa Leseni 377 zinazohusu huduma za Usafiri wa Baharini pamoja na kufanya Ukaguzi wa Meli 95.

iii. Kupitia Sheria ya ZMA namba 3 ya mwaka 2009, kutayarisha Kanuni 3 na Miongozo 4 (Standard Operating Procedures - SOP) ya kufanyia kazi.

iv. Kufanya Mikutano na Wadau wa Sekta ya Usafiri Baharini na kuwaelimisha Wananchi kwa kufanya vipindi vya TV na Redio juu ya utunzaji wa mazingira ya bahari na usalama wa usafiri wa baharini.

v. Kuendelea kuzifanyia kazi hoja za ukaguzi wa IMSAS kwa mujibu wa Mpango wa Marekebisho ulioandaliwa.

vi. Kuendelea kusimamia utatuzi wa changamoto za Mabaharia pamoja na maslahi yao.

vii. Kufanya mapitio ya muundo wa ZMA pamoja na majukumu ya Idara, vitengo na divisheni na kuhakikisha yanaendana na malengo ya Taasisi.

viii. Kuwajengea uwezo Wafanyakazi 39 wa Mamlaka pamoja na kuimarisha mazingira ya kutendea kazi.

ix. Kusimamia utoaji wa vyeti vya Mabaharia wanaosoma chuo cha ubaharia cha SUZA

**Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**86. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mamlaka ya Usafiri Baharini imekadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 8,797,036,295** na imepanga kutumia jumla ya **Shilingi. 8,463,979,092** kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, jumla ya **Shilingi 2,361,420,680** ni **Shilingi 6,425,615,615** kwa kazi za kawaida.

**E.3. SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR**

**87. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bandari limepewa jukumu la kutoa huduma za uingizaji na utoaji meli katika Bandari za Unguja na Pemba, ufungaji na ufunguaji wa meli kwenye gati, uangalizi wa alama za kuongozea usafiri wa meli (minara na maboya), uteremshaji na upakiaji wa bidhaa kwenye meli pamoja na vyombo vyengine vya usafiri wa baharini.

**Utekelezaji wa kazi za Shirika kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**.

**88. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 Shirika la Bandari limefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

**a. Huduma za Bandari:** Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025, Shirika limehudumia vyombo mbali mbali vya mizigo na abiria kwa kushirikiana na wawekezaji katika bandari za Unguja na Pemba. Jumla ya meli za kigeni 152 zenye uzito wa GRT 1,385,574 zilihudumiwa sawa na asilimia 95 ya makadirio ya meli 160 zilizopangwa kwa mwaka 2024/2025.

Kwa upande safari za Meli za ndani zilizohudumiwa ni 5,694 sawa na asilimia **79** ya makadirio ya meli 7,200 zilizopangwa kuhudumiwa kwa mwaka 2024/2025. Aidha, jumla ya majahazi

7,860 yamehudumiwa sawa na asilimia **63.4** ya majahazi 12,400 yaliyopangwa kuhudumiwa katika kipindi cha mwaka 2024/2025. **Kiambatanisho nambari 10 A kinahusika**.

Kwa upande wa huduma za mizigo, Shirika limehudumia jumla ya Tani 1,107,455 za mizigo mchanganyiko sawa na asilimia 58.9 ya makadirio ya Tani 1,881,645 zilizopangwa kuhudumiwa katika mwaka wa fedha 2024/2025. Ikiwa Tani 724,643 za mizigo ya meli na Tani 382,812 za mizigo ya majahazi.

Kwa upande wa Mizigo ya Makontena Shirika limehudumia Makontena 40,334 sawa na asilimia 59 ya makadirio ya makontena 68,360 yaliyopangwa kuhudumiwa katika mwaka wa fedha 2024/2025. Makontena hayo yamehudumiwa katika bandari ya Malindi, Fumba, Mkoani na Wete. Aidha, Shirika kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025 limehudumia Mafuta ya kuwasha (Petroleum product) lita 175,489,223. **Kiambatanisho namba 10 B kinahusika.**

**b. Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**89. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha, 2024/2025, Shirika la Bandari limefanikiwa kutekeleza Miradi ifuatayo:-

i. **Ujenzi wa Bandari ya Shumba:** Shirika la Bandari linaendelea na ujenzi wa Bandari ya Shumba Mjini itakayohudumia abiria na mizigo pamoja na kuhudumia meli zenye uzito wa Tani 2,000. Mradi huu unatekelezwa katika awamu mbili. Awamu ya Kwanza inajumuisha ujenzi wa gati yenye urefu mita 45 na upana 20 na kazi hiyo inatekelezwa na Mkandarasi Comfix Engineering kwa gharama ya Shilingi 5,772,506,880.00. Hadi kufikia Machi, 2025, kazi ya ujenzi wa gati imekamilika na hatua inayoendelea kwa sasa ni kukamilisha uwekaji wa nguzo za kufunga kamba ya meli (Bollard) na kinga za ukuta wa meli (Fender) pamoja na uwekaji wa miundombinu ya maji na umeme, utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 91. Hadi kufikia Machi 2025, Mkandarasi ameshalipwa Shilingi 5,145,948,889.35 sawa na asilimia 89 ya gharama za mradi.

Awamu ya Pili ya Mradi huu inatekelezwa na Kampuni ya Scenic Construction and Consultancy ltd kwa ajili ya kujenga uzio wa bandari wenye urefu wa mita za mraba 960, Msikiti na Banda la Abiria. Kazi za ujenzi zinaendelea ambapo ujenzi wa uzio umefikia asilimia 90, ujenzi wa msikiti ambao unajengwa katika eneo la nje la bandari kwa ajili ya usalama umefikia asilimia 50 na Jengo la Abiria limefikia asilimia 10. Kazi za ujenzi zinatarajiwa kukamilika Mwezi wa Disemba, 2025. Awamu ya pili hadi kukamilika kwake inatarajiwa kutumia jumla ya Shilingi 11,656,329,930.50 na hadi kufikia mwezi wa Machi, 2025 jumla ya Shilingi 719,963,366.9 zimetumika sawa na asilimia 6.2. Kazi za ujenzi wa Bandari ya Shumba zinasimamiwa na Kampuni ya Annova Consultancy.

ii. **Ujenzi wa Bandari ya Wete:** Kazi ya upembuzi yakinifu katika Bandari ya Wete imemaliza ambapo Mshauri Elekezi Inros Lackener kutoka Ujerumani amefanya Upembuzi yakinifu na Usanifu wa Awali (Feasibility Study and Preliminary Engineering Design) na ametayarisha Tender Document na Mchoro ambapo taarifa inaonesha kutachimbwa baharini (Dredging) kwa urefu wa mita za mraba 6.5 badala ya 8.5 ili kuhudumia meli zenye ukubwa (DW) 1,000, kina cha maji chenye urefu wa mita za mraba 4.0, jengo la abiria lenye uwezo wa kuhudumia abiria 2,000. Kwa sasa Taasisi kutoka nchini Korea - KOICA na baadhi ya wawekezaji wameonesha nia ya kuwekeza katika bandari hiyo. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa Dola za Kimarekani 359,575 sawa na Shilingi 845,001,250.00 hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya Shilingi 279,117,900.00 zimetumika.

iii. **Uimarishaji wa Bandari ya Mkoani:** Shirika la Bandari inaendelea na maboresho ya Bandari ya Mkoani ambayo ipo chini ya Fumba Port kwa kuanza na ujenzi wa Jengo la Abiria, Ofisi, Maghala (Warehouse) na utanuzi wa Bandari Kavu ambapo itakamilika ndani ya miezi 18 kwa gharama za Dola za Kimarekani 3,500,000. Pia Shirika

la Bandari katika kuimarisha huduma katika Bandari ya Mkoani imenunua Baji (Tishali) ambalo limeshafungwa katika Bandari hiyo na litarahisisha safari za boti baina Unguja, Pemba na Tanga zinazotarajiwa kuanza rasmi Mwezi wa Mei, 2025. Gharama za ununuzi zilizopangwa kutumika ni Shilingi 1.2 Bilioni na hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya Shilingi 621,000,000 zimetumika.

iv. **Mradi wa Uwekaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Uendeshaji wa Bandari (E-Port):** Shirika linaendelea na utaratibu wa kuweka mifumo ya kielektroniki (E-Port) kwa ajili ya kuimarisha huduma zake na kuongeza ufanisi katika utawala, uendeshaji wa vyombo na uhudumiaji mizigo. Mfumo huo una module kuu 5 zikiwemo Mfumo wa Kusimamia Rasilimali za Taasisi (Enterprise Resources Planning), mfumo wa usimamizi na uongozaji wa vyombo vya baharini (Vessel Tracking System), mfumo wa usimamizi wa huduma za mizigo (Terminal Operating System), mfumo wa usimamizi wa matumizi ya mafuta katika Shirika (Fleet and Fuel Management System) na mfumo wakutoa muhtasari wa ripoti juu ya shughuli zote za kiutendaji (E-Portal).

Mradi huu unatekelezwa na Kampuni ya Fotris na Watsila ikisimamiwa na mshauri elekezi Kampuni ya Aims and Tradelogic kutoka Mombasa Kenya. Mradi umefikia asilimia 85 ambapo mifumo mitatu kati ya mitano tayari imekamilika nayo ni mfumo wa ERP, TOS na FFMS . Mifumo ambayo bado haijakamilika ni VTS na E-PORTAL. Kwa sasa Shirika linategemea kupokea vifaa kwa ajili ya ujenzi wa "VTS tower" na limepeleka wafanyakazi 12 nchini Uturuki kwa ajili ya kujifunza mifumo ya uendeshaji ikiwemo Mfumo wa VTS. Hadi kufikia Machi, 2025 jumla Shilingi 14,509,436,364 sawa na Dola za Kimarekani 5,000,000 zimetumika.

v. **Ujenzi wa Bandari ya Mpiga Duri:** Mradi wa Bandari ya Abiria ya Maruhubi ni miongoni mwa miradi mikuu ya kimkakati ambayo imeanzishwa na Serikali ya Mapinduzi

ya Zanzibar kupitia Shirika la Bandari katika juhudi za kukuza na kuinua kiwango cha huduma katika Sekta ya Usafiri wa Baharini. Mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano na Kampuni ya ZF Devco na utajumuisha, Baji (Tishali) kwa meli za mwendokasi, Kituo cha Kuegesha Vyombo vya RoRo, Jengo Jipya la Abiria, Maghala, Eneo Maalum la Kiuchumi lenye huduma za burudani na malazi, vituo vya biashara vya B2B, kituo cha ndege za baharini, kituo cha mabasi na vituo vya biashara. Mradi utajengwa katika awamu tatu ndani ya kipindi cha mkataba wa ukodishaji. Ujenzi umeanza kwa awamu ya kwanza kwa kuendelea na ujenzi wa gati za meli za RORO ili kupunguza foleni katika Bandari ya Abiria ya Malindi. Awamu ya Kwanza inatarajiwa kukamilika mwezi wa Septemba, 2025. Gharama za mradi huu hadi kukamilika kwake ni Dola za Kimarekani 400,000,000.

vi. **Ujenzi wa Bandari ya Abiria Malindi.** Mradi huu unahusisha ukarabati wa Bandari ya Abiria ya Malindi utakaofanyika kwa kushirikiana na Kampuni ya ZF Devco kupitia mkataba maalum wa makubaliano ili kuifanya bandari ya kileo. Mradi huu utajumuisha ukarabati wa sehemu ya kukaa abiria wanaosafiri, ukarabati wa jengo la watu mashuhuri (VIP lounge), ujenzi wa Mkahawa, Maduka ya Biashara, Maegesho ya Vyombo Baharini kwa ajili ya kuhudumia wasafiri wanaokwenda visiwani, uhamishaji wa bandari ya meli za RoRo kwenda Mpigaduri pamoja na uwekaji wa miondombinu ya umeme wa kutumia nguvu za jua. Gharama za Mradi huu ni Dola za Kimarekani 5,000,000.

vii. **Ujenzi wa Gati katika Bandari ya Fumba:** Mradi wa ujenzi wa gati katika Bandari ya Fumba ni muendelezo wa marekebisho katika bandari hiyo ili kuweza kuhudumia meli za makontena muda wote ili kuondokana na kusubiria maji au kutumia meli za land craft tu. Gati hiyo itakuwa na urefu wa mita 340 kutoka nchi kavu, urefu wa gati (kichwa cha gati) ni mita 225 na upana

wa mita 25, urefu wa gati upande wa ndani ni mita 141 na kina cha maji kitakuwa mita 12 wakati wa maji ya chini (maji ya juu ni mita 14 hadi 15). Itakuwa na uwezo wa kuhudumia meli mbili zenye LOA (Length Overall) ya mita 200 na mita 140. Aidha, hadi kufikia Machi, 2025 kumefanyika tathmini ya malipo ya fidia kwa wakaazi waliopo katika eneo la mradi kutokana na kuongezeka kwa eneo la mradi.

viii. **Ujenzi wa Bandari ya Kizimkazi:** Mradi huu ni miongoni mwa miradi ya kimkakati inayotekelezwa ili kuimarisha uchumi wa Zanzibar, Pia unalenga kuboresha huduma za usafiri wa baharini na kuongeza fursa za ajira kwa wakazi wa eneo hilo. Bandari hii itaweza kutoa huduma za "sea taxi" ambazo tayari kuna mashirikiano na Kampuni ya Infinity na Kampuni ya ZF Devco kwa ajili ya kazi za usanifu (Design) wa Vituo hivyo. Hivyo, uwepo wa bandari hii utaweza kuufungua Mkoa wa Kusini kiutalii na kurahisisha safari za Kusini kwenda Mjini pamoja na Tanzania bara.

ix. **Miundombinu ya Ushushaji wa Mafuta na Gesi (CBM) Mangapwani:** Mradi wa Bomba la Mafuta Bandarini (CBM) wa Mangapwani ni sehemu muhimu ya Mpango Mkuu wa Mangapwani (Masterplan) wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Lengo la mradi huu ni kuanzisha miundombinu ya kisasa ya kupakua na kupakia mafuta na gesi ili kuboresha usambazaji wa mafuta na gesi Zanzibar. Ujenzi wa miundombinu hii mipya ya kuhifadhi na kushusha mafuta utaondoa changamoto za usambazaji na gharama za upakiaji kwa mahitaji ya ndani na kuiwezesha Zanzibar kufanya biashara ya kupeleka visiwa jirani kama Comoro, Madagasca na nyenginezo. Mradi huu utatekelezwa na Kampuni ya Offshore Mooring Ltd (Tanzania) ambao utagharimu jumla ya Dola za Kimarekani 17,000,000. Mradi huu unatekelezwa kwa muda wa Miezi 15 na unatarajiwa kukamilika Septemba, 2025, Eneo la Ujenzi lina ukubwa

wa mita za mraba 2000. Mradi huu utajumuisha Mfumo wa maboya na kiungo cha ushushaji na kupakia (PLEM), kiunganishi cha Bomba za Mafuta (Manifold), mita za kupimia kiwango cha mafuta (Flowmeter) na Afisi za wadau wa bandari na huduma za upakiaji na ushushaji wa mafuta.

x. **Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Taxi za Baharini:** Mradi huu utahusisha uwekaji wa Vituo vya Taxi katika maeneo ya bandari mbali mbali na Visiwa. Miongoni mwa maeneo ambayo Vituo hivyo vitajengwa ni Malindi, Africa House, Fumba Town (CPS), Maruhubi (ZF Devco & Verde) Mangapwani (Sea Cliff), Mkokotoni, Nungwi Mnarani na Kizimkazi. Kwa upande wa Visiwa utajumuisha visiwa vya Bawe, Chumbe, Kwale, Changuu, Pungume, Tumbatu na Uzi kwa upande wa Unguja na kwa upande wa Pemba utatekelezwa katika vituo vya Mkoani, Wesha, Wete, Shumba, Makangale, Misali. Kwa sasa tayari kuna mashirikiano na Kampuni za Infinity na ZF Devco kwa ajili ya kufanya usanifu na ujenzi wa Vituo hivyo.

**Mapato na Matumizi**

**90. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Shirika la Bandari limekadiria kukusanya jumla ya **Shilingi. 37,962,452,234.52** kupitia katika vyanzo vyake mbalimbali. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 Shirika lilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 23,838,238,043.60.** Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **Shilingi 27,665,931,140.30** zimekusanywa sawa na asilimia **116** kwa makadirio ya miezi tisa na asilimia **73** ya makadirio kwa mwaka.

Kwa upande wa matumizi, Shirika la Bandari kwa mwaka wa fedha 2024/2025 lilipanga kutumia jumla ya **Shilingi 77,441,297,397.27** ikiwa **Shilingi 16,782,737,922.00** kwa matumizi ya kawaida **(Shilingi 8,021,731,452.00** kwa matumizi ya kawaida na **Shilingi 8,761,006,470.00** kwa ajili

ya stahiki za wafanyakazi) na **Shilingi 60,658,559,475.27** kwa matumizi ya Miradi ya maendeleo. Shirika lilijipangia kuchukua mkopo wa **Shilingi 40,000,000,000** kwa ajili ya kukabiliana na bajeti ya miradi.

Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **Shilingi 21,326,882,325.74** zimetumika sawa na asilimia 89 ya makadirio ya **Shilingi 23,880,300,409** zilizopangwa kwa kipindi cha miezi tisa. Kati ya fedha hizo **Shilingi 8,057,983,043.38** zimetumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo, **Shilingi 10,336,370,963.67** kwa matumizi ya kazi za kawaida, **Shilingi 850,000,000** ni gawio la Serikali, **Shilingi 337,500,000** na **Shilingi 1,745,028,318.69** ni malipo ya TRA.

## MALENGO YA SHIRIKA LA BANDARI YANAYOTARAJIWA KUTEKLEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**91. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Shirika la Bandari limepanga kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuhudumia Meli za ndani zipatazo 11,000 na Majahazi 12,000.

ii. Kuhudumia tani 2,485,000 za Mzigo Mchanganyiko na Makontena (TEUS) 105,000 pamoja na Lita 286,138,380 za mafuta ya kuwasha (Petroleum Fuel).

iii. Kuendelea kukamilisha miradi inayoendelea ikiwemo Ujenzi wa Bandari ya Shumba Mjini, Kizimkazi, Ujenzi wa Bandari Kavu, ujenzi wa gati katika Bandari ya Fumba na Uimarishaji wa Bandari ya Mkoani ikiwemo kujenga Jengo la Abiria na Ofisi, Ujenzi wa Bandari ya abiria Mpiga Duri, kujenga maeneo ya Vituo vya Usafiri wa Baharini (sea taxi stations).

iv. Kufanya ukarabati wa minara, maboya na becon pamoja kufanya manunuzi ya tagi na "Pilot" boti, gari, mashine ya upekuzi wa mizigo, maboya ya kuongozea meli, vifaa vya TEHAMA pamoja na vifaa vya kudhibiti umwagikaji wa mafuta baharini.

v. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ili waweze kufanyakazi zao kwa ufanisi.

**Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**92. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Shirika la Bandari Zanzibar limekadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 45,930,497,190.33** na kutumia jumla ya **Shilingi 63,520,197,971.75** ikiwa **Shilingi 14,475,352,789.12** kwa kazi za kawaida **Shilingi 8,731,364,013.94** kwa ajili ya maslahi ya wafanyakazi na **Shilingi 40,313,481,168.69** kwa kazi za maendeleo. Kufanikisha matumizi haya Shirika litalazimika kuchukua mkopo wa **Shilingi**.**15,000,000,000** ili kuzitekeleza baadhi ya shughuli za miradi.

## E.4. SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR

**93. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Meli Zanzibar linamilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Shirika hili lilianzishwa rasmi chini ya Sheria nambari 3 ya Mwaka 2013 (The Zanzibar Shipping Corporation Act, 2013) na limepewa jukumu la kuzisimamia na kuziendesha meli zote za Serikali pamoja na kutoa huduma za Uwakala kwa Meli za Kigeni zinazoingia katika Bahari ya Zanzibar.

**Utekelezaji wa Kazi za Shirika kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.**

**94. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Shirika la Meli Zanzibar limefanikiwa kutekeleza yafuatayo: -

a. **Matengenezo ya Meli ya MV Mapinduzi II**. Shirika la Meli linaendelea kuifanyia matengenezo makubwa meli ya MV Mapinduzi II kwa kutumia Kampuni ya Kookje Engineering ya Korea. Matengenezo ya Meli hiyo yanajumuisha Mashine zote za meli ambazo tayari zimeshatengenezwa na zinafanya kazi vizuri. Hadi kufikia Mwezi wa Machi, 2025 Matengenezo ya Meli hiyo

yamefikia asilimia 90. Meli hiyo imeshafanyiwa majaribio (Sea Trials) mara 4 kwa mafanikio ikiwemo majaribio makubwa ambapo meli ilitoka Unguja na kwenda Kisiwa cha Pemba na kurudi Unguja. Kwa sasa meli inatarajiwa kupelekwa Chelezoni, Mombasa, Kenya mwezi wa Mei, 2025 endapo meli zilizopo Chelezoni kwa sasa zitamaliza matengenezo yake. Miongoni mwa kazi zitakazofanyika huko ni pamoja na kusafisha sehemu ya chini ya meli, kurekebisha 'valves' zinazotumia upepo (Pneumatic valves), kupakwa rangi na kuangalia kama kutakuwa na uhitaji wa matengenezo mengine.

b. **Utoaji wa Huduma za Kusafirisha Mafuta kwa Kutumia Meli ya MT Ukombozi II:** Meli ya MT Ukombozi II inaendelea kufanya kazi vizuri ya kusafirisha mafuta kutoka Tanga na Dar es Salaam kuja Zanzibar. Meli hii inaendelea kukodiwa kwa kodi ya safari (Voyage Charter) na Kampuni ya GBP Tanzania. Meli ya MT Ukombozi II kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2024 imefanya jumla ya safari 30 sawa na asilimia 100 ya safari 30 zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Jumla ya Shilingi 3,900,000,000 zimepatikana kutokana na safari hizo.

c. **Utoaji wa Huduma za Uwakala wa Meli:** Shirika linaendelea kutoa huduma za uwakala wa meli. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya meli 155 za kigeni zimehudumiwa, kati ya meli 174 zilizopangwa sawa na asilimia 89 ya makadirio. Meli hizo ni pamoja na meli za kuchukua Makasha, Mafuta, Gesi, Kijeshi, Kichele na Kitalii.

d. **Ujenzi wa Boti Mbili za Abiria za Mwendo wa Kasi:** Wizara kupitia Shirika la Meli limeanza utaratibu wa ujenzi wa boti mbili za mwendo wa kasi zitakazofanya kazi baina ya Unguja, Pemba, Tanga na Dar es Salaam. Mkataba wa Ujenzi wa Boti hizo umetiwa saini tarehe 17 Julai, 2024 baina ya Shirika la Meli na Kampuni ya Synergy Shipbuilder ya India ambayo ndio Mjenzi wa boti hizo. Mjenzi huyo ameshalipwa Malipo ya

Utangulizi (Advanced Payment) na pia ameshalipwa malipo ya Awamu ya Kwanza (First Installment). Boti hizi zitakuwa na uwezo wa kuchukuwa abiria 650 kwa kila moja. Kutokana na kutokea changamoto mbali mbali za taratibu za ununuzi na upatikanaji wa mkopo wa ujenzi wa boti, ujenzi umechelewa kidogo. Kwa sasa Mkandarasi ameshakusanya vifaa vyote vinavyohitajika na kazi ya uwekaji wa Mkuku (Keel laying) inatarajiwa kufanyika mwezi wa Mei, 2025. Boti hizi zinatarajiwa kuwasili nchini Mwezi wa Juni, 2026.

**Mapato na Matumizi**

**95. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Shirika la Meli lilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 14,102,265,605** kutoka katika vyanzo vyake. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Shirika lilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 10,689,752,284** na hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **Shilingi 11,072,709,955** zimekusanywa sawa na asilimia **104** ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Shirika la Meli lilipanga kutumia jumla ya **Shilingi 13,829,214,214** kwa matumizi ya kazi kawaida.Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Shirika lilipanga kutumia jumla ya **Shilingi 10,581,186,104** na hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **Shilingi 7,710,620,885** zimetumika sawa na asilimia **73** ya makadirio.

**MALENGO YA SHIRIKA LA MELI YANAYOTARAJIWA KUTEKLEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

**96. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Shirika limepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuanza kwa safari za kusafirisha abiria na mizigo kwa kutumia Meli ya MV Mapinduzi II. Jumla ya abiria 76,800 wanatarajiwa kusafirishwa na tani 24,000 za mizigo zinatarajiwa kuchukuliwa baina ya Visiwa vya Unguja na Pemba.

ii. Kuendelea na ujenzi wa boti mbili za mwendo wa kasi ambazo zitafanya kazi ya usafirishaji abiria baina ya Unguja, Pemba, Tanga na Dar es salaam.
iii. Kuendelea kutoa huduma za uwakala kwa meli zote zinazokuja katika bahari ya Zanzibar ambapo Shirika limepanga kuhudumia makasha 34,643 na Meli 214 zinazochukua Makasha, Mafuta, Gesi, Kijeshi, Mizigo Kichele na Kitalii.
iv. Kuipeleka Meli ya MT Ukombozi II chelezoni Mombasa, Kenya kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi.
v. Kuendelea kuyafanyia matengenezo majengo ya Afisi Makao Makuu na Dar es Salaam.
vi. Kuwajengea uwezo wafanyakazi 35 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa tija na ufanisi.

**Makadirio ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**97.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Shirika limekadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 14,373,657,800** kupitia vyanzo vyake vya mapato. Kwa upande wa matumizi, Shirika limepanga kutumia **Shilingi 13,062,991,200** kwa kazi za kawaida na **Shilingi 648,600,000** kwa kazi za Maendeleo.

**E.5. MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR**

**98.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imeanzishwa kwa Sheria Namba 8 ya Mwaka 2011 na ina jukumu la kuviendesha, kuvisimamia na kuvitunza Viwanja vya Ndege vya Serikali pamoja na kusimamia usalama wa Safari za Abiria, Ndege na Mizigo katika Viwanja vya Ndege vya Serikali. Aidha, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wakati wa utekelezaji wa majukumu yake inazingatia taratibu na Sheria zote za uendeshaji wa viwanja kama zinavyoelekezwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (Tanzania Civil Aviation Authority (TCAA)) na International Civil Aviation Organization (ICAO).

**Utekelezaji wa Kazi za Mamlaka kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.**

**99. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imefanikiwa kutekeleza yafuatayo: -

a. **Kuhudumia Safari za Ndege,** Abiria na Mizigo: Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inaendelea kutekeleza kazi zake za kawaida za kuhudumia safari za ndege, abiria na mizigo katika Viwanja vya Ndege Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, jumla ya safari za ndege 55,965 zimehudumiwa sawa na asilimia 104 ya makadirio ya safari 53,754 zilizopangwa kuhudumiwa kwa mwaka 2024/2025. Kati ya safari hizo, safari za ndege 51,597 zilihudumiwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abedi Amani Karume na safari za ndege 4,368 zilihudumiwa katika Uwanja wa Ndege wa Pemba. Safari za ndege za Kimataifa zilikuwa ni 11,180 na safari za ndani zilikuwa ni 40,388. **Kiambatanisho namba 11 A kinahusika.**

Kwa upande wa huduma za Ndege, Mamlaka imehudumia jumla ya Mashirika na Kampuni za ndege 71 za ndani na nje katika Viwanja vya Ndege vya Zanzibar katika kipindi cha miezi tisa. **Kiambatanisho namba 11 B kinahusika**.

Aidha, jumla ya abiria 1,994,360 wamehudumiwa sawa asilimia 140 ya makadirio ya abiria 2,420,384 waliopangwa kuhudumiwa kwa mwaka 2024/2025. Kati ya hao, Abiria, 1,914,055 walihudumiwa katika Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume na abiria 80,330 walihudumiwa katika Uwanja wa ndege wa Pemba. Kati ya abiria hao, abiria 1,186,402 ni wa safari za kimataifa na abiria 807,958 ni wa safari za ndani. Jumla ya Abiria waliopita (transit passengers) ni 167,865 ikiwa abiria 167,798 walipita katika Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume na abiria 67 walipita katika Uwanja wa ndege wa Pemba. **Kiambatanisho namba 11 C kinahusika.**

Kwa upande wa mizigo, jumla ya tani 3,432 zilihudumiwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume sawa na asilimia 99 ya tani 3,459 zilizokadiriwa kwa mwaka 2024/2025.

b. **Kuimarisha Ulinzi na Usalama wa Viwanja vya Ndege Unguja na Pemba**: Katika kuimarisha ulinzi na usalama wa Viwanja vya Ndege, kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imefanikiwa kufanya matengenezo ya kawaida (service) ya mashine na milango (WTMD) 17 kwa Uwanja wa Ndege wa AAKIA na Pemba, kununua Camera za CCTV zipatazo 15 za aina ya Bullet Camera (12Pcs) na Dome Camera (Pcs 3) katika Uwanja wa Pemba. Aidha, Mamlaka ilipanga kuwapatia mafunzo ya ulinzi na usalama wafanyakazi 217 na hadi kufikia Machi, 2025 imefanikiwa kuwapatia mafunzo ya ulinzi na usalama wafanyakazi 184 sawa na asilimia 84.7 ya wafanyakazi waliopangiwa kupatiwa mafunzo hayo. Mafunzo hayo yametolewa katika fani tofauti kama ifuatavyo:- wafanyakazi 107 wamepatiwa mafunzo ya “basic screener”, “refreshers screener” pamoja na “interview” na kupatiwa leseni, “cargo and mail” kwa wafanyakazi watatu (3), “inspectors” kwa mfanyakazi 1, mafunzo ya kufunga “finding za ICAO phase III” kwa wafanyakazi 71 pamoja na “risk assessment management” wafanyakazi wawili (2). Lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha wafanyakazi kutoa huduma bora na zenye ufanisi.

c. **Ukarabati wa Jengo la Abiria la Terminal 1:** Jengo la abiria la TB 1 ni jengo la mwanzo la abiria lililojengwa miaka ya 1950 likiwa na mnara wa kuongozea ndege (Control Tower). Kwa muda mrefu, Jengo hilo limekuwa linatumika kama jengo la Ofisi Kuu za Mamlaka ya Viwanja Vya Ndege Zanzibar pamoja na eneo la Wageni Mashuhuri na Viongozi Wakuu wa Nchi (Presidential VIP). Kutokana na kuchakaa kwa jengo hilo pamoja na ongezeko la uhitaji wa uwepo wa Huduma za Ndege Binafisi

(Private Jet Operation), uhitaji wa huduma za kipekee kwa Wageni Mashuhuri wa kibiashara (Commercial Important Persons) na uhitaji uboreshaji wa huduma za Wageni Mashuhuri na Mashuhuri Zaidi (VIP na VVIP), Serikali imeamua kulifanyia usanifu na maboresho makubwa jengo hilo pamoja na kulifanyia utanuzi ili liendane na hadhi za Kimataifa. Jengo hilo litakuwa na kumbi mbili ambazo zitahudumia wageni kutokana na hadhi na madaraja yao. Baada ya kukamilika ujenzi, tunategemea kuwa jengo bora la VIP katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati na kuleta ushindani wa kidunia katika kuhudumia Watalii na Wageni wa Daraja la Juu. Usanifu, Ukarabati na Ujenzi wa Jengo la Abiria TB1 umeanza rasmi tarehe 18 Mei, 2024 na unatarajiwa kukamilika ndani ya Mwaka 2025. Mkandarasi wa jengo hili ni Kampuni ya Estim Enterprises Limited. Kwa ujumla ukarabati na ujenzi wa jengo la TB1 unaendelea kwa kasi kubwa na hadi kufikia Mwezi wa Machi, 2025 ujenzi huo umefikia asilimia 84 ya utekelezaji.

d. **Ujenzi wa Kituo cha Biashara (Business Center) Katika Jengo la Terminal 3,** Mamlaka imefanikiwa kuimarisha mazingira ya biashara katika Uwanja wa AAKIA kwa kuingia Mkataba na Kampuni ya Estim Enterprise kwa ajili ya kujenga na kuendesha Kituo cha Biashara (Business Center) katika Uwanja wa AAKIA. Aidha ujenzi huu utajumuisha ujenzi wa Ofisi, eneo kwa huduma za Mabenki, Maduka na Mikahawa. Ujenzi huu umeanza rasmi tarehe 17 Aprili 2024 na unatarajiwa kukamilika tarehe 16 Novemba, 2025. Ujenzi unaendelea vizuri na hadi kufikia Mwezi wa Machi, 2025 umefikia asilimia 60 ya utekelezaji.

e. **Kuweka Mfumo Maalum wa Kuongozea Ndege Wakati wa Kutua (Instrument Landing System – ILS) na Uwekaji wa Taa (Precision Approach Lights):** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Mamlaka ya Anga Tanzania (TCAA) ilianzisha Mradi wa Uwekaji

wa Mfumo Maalum wa Kuongozea Ndege unaoitwa "Instruments Landing System" (ILS) ambao humsaidia rubani wakati wa kutua hasa wakati wa usiku na hali mbaya ya hewa. Mradi huo umehusisha uwekaji wa Mitambo na Taa Maalum zinazoitwa "Precision Approach Lights". Uwekaji wa taa hizi umeanza tarehe 03 Septemba,2024 na kukamilika 30 Novemba, 2025 na kazi ya uwekaji wa taa umefanywa na Kampuni ya ADB SAFEGATE kutoka Afrika Kusini. Jumla ya taa mpya 136 zimewekwa. Mradi umehusisha uchimbaji wa mashimo (manholes) kwa ajili ya kuweka miundombinu ya umeme, kuchimba misingi kwa ajili ya kupitisha bomba za miundombinu ya umeme, kuunganisha mifumo ya taa na mifumo ya Airtraffic Control tower (ATC) pamoja na kufanya majaribio kabla ya kuanza kutumia taa mpya. Mradi huu utasaidia ndege kutua katika hali yoyote ya hewa ikiwa mvua, ukungu au hata kiza kinene.

f. **Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Paje:** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mamlaka ya Viwanja vya ndege tayari imeanza hatua za awali za kulitambua na kulipima eneo litakalotumika kwa ajili ya Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Paje. Aidha eneo lenye ukubwa wa mita za mraba (2000x400) limetambuliwa na kupimwa, hatua inayofuata ni kuekewa alama (beacon) ili kuruhusu harakati za ujenzi kuanza.

**Mapato na Matumizi**

**100. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 51,508,339,684** na kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 41,206,671,744** kupitia vyanzo vyake vya ndani. Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya **Shilingi 36,181,204,123.34** zimekusanywa sawa na asilimia **88** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **70** ya makadirio ya mwaka.

**101. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ilipanga kutumia jumla ya **Shilingi 51,508,339,684** kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo na kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 ilikadiria kutumia jumla ya **Shilingi 40,850,582,326**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 13,282,831,384** ni mshahara, **Shilingi 20,380,987,300** ni kwa matumizi mengineyo na **Shilingi 17,844,521,000** kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2025, jumla ya **Shilingi 35,124,636,572.27** zimetumika sawa na asilimia **85** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **68** ya makadirio ya mwaka, Kati ya fedha hizo **Shilingi 9,346,450,133.7** ni mshahara, **Shilingi 12,288,105,569.07** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 13,490,080,869.51** ni kwa kazi za maendeleo.

## MALENGO YA MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR YANAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**102. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama ili kukidhi Viwango vya Kitaifa na Kimataifa kwa kuvifanyia matengenezo Vifaa vya Ulinzi na Usalama pamoja na kuwapatia mafunzo ya Ulinzi na Usalama wafanyakazi 155 wa Kitengo cha ulinzi na usalama.

ii. Mamlaka imepanga kuimarisha miundombinu kwa kukamilisha ujenzi na matengenezo ya Jengo la Abiria (Terminal 1), kukamilisha ujenzi wa Awamu ya Kwanza ya Jengo la Abiria (Terminal 2) katika Uwanja wa AAKIA, kuanza jenzi wa Jengo Jipya la Abiria la (TB 2) awamu ya pili, kuanza kwa ujenzi wa maegesho ya ndege (Remote Apron) katika uwanja wa ndege wa AAKIA, kuanza kwa ujenzi wa Mnara wa Kuongozea Ndege, ukarabati wa Mabega ya Barabara ya Kurukia Ndege (Runway Shoulders) katika Uwanja wa AAKIA, kuanza ujenzi wa

Jengo la Ofisi za Mamlaka kwa hatua za awali pamoja na kuanza Awamu ya Kwanza ya maboresho ya Uwanja wa Ndege wa Nungwi. Mamlaka imepanga kununua gari moja ya zimamoto katika Kiwanja cha AAKIA.

iii. Kukamilisha ujenzi wa Kituo kipya cha Biashara (Bussiness Centre) katika Jengo la Abiria la TB 3.

iv. Mamlaka imepanga kuhudumia abiria 2,321,400, Ndege 70,294 na Mzigo tani 3,543 katika Viwanja vya Ndege Unguja na Pemba.

**Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**103. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imekadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 55,395,962,119** kupitia vyanzo vyake vya mapato na imepanga kutumia jumla ya **Shilingi 55,395,962,119**. Kati ya hizo, **Shilingi 39,536,449,513** kazi za kawaida na **Shilingi 15,859,512,606** kwa kazi za maendeleo.

## E.6 BODI YA USAJILI WA WAKANDARASI.

**104. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Usajili wa Wakandarasi ina jukumu la kusajili Wakandarasi na kutunza Daftari la Wakandarasi, kusimamia shughuli za Wakandarasi, kupanga na kutoa Mafunzo, Warsha, Makongamano juu ya masuala yanayohusiana na ujenzi, kuweka vigezo na madaraja mbalimbali ya Wakandarasi kwa ajili ya usajili pamoja na kupokea, kuchunguza na kusikiliza malalamiko dhidi ya Wakandarasi.

**105. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

a. **Usajili wa Wakandarasi Wapya:** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi ilikadiria kusajili Wakandarasi wapya 56 na hadi kufikia Machi, 2025 imefanikiwa kusajili Wakandarasi wapya 66 sawa na asiliamia 118 ya makadirio ya mwaka.

b. **Usajili wa Miradi:** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Bodi ilipanga kusajili miradi 220 na hadi kufikia Machi, 2025 imefanikiwa kusajili miradi 398 sawa na asilimia 178 ya makadirio ya mwaka.

c. **Ukaguzi wa Miradi:** Kwa Mwaka 2024/2025, Bodi ilipanga kukagua miradi 100 na hadi kufikia Machi, 2025 imefanikiwa kufanya ukaguzi wa miradi 361 sawa na asilimia 361 ya makadirio ya mwaka. Aidha, Bodi imechukuwa hatua za kisheria na kinidhamu kwa Wakandarasi 154 waliokiuka sheria.

**Mapato na Matumizi**

**106. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 804,000,000** na kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 642,616,250.** Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya **Shilingi 1,379,246,000** zimekusanywa sawa na asilimia **215** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **172** ya makadirio ya mwaka.

Kwa upande wa matumizi, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi ilikadiria kutumia jumla ya **Shilingi 402,000,000** na kwa kipindi cha miezi tisa ilikadiria kutumia **Shilingi 286,445,500.** Hadi kufikia Machi, 2025 jumla **Shilingi 221,261,973** zimetumika sawa na asilimia **77** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **55** ya makadirio ya bajeti yanayotokana na makusanyo ya bodi.

**MALENGO YANAYOTARJIWA KUTEKLEZWA NA BODI YA USAJILI WA WAKANDARASI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.**

**107. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha, 2025/2026, Bodi ya Usajii wa Wakandarasi imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuendelea kusajili Wakandarasi wapya 72 na kuwapandisha madaraja Wakandarasi ambao walishasajiliwa na Bodi.

ii. Kuendelea na usajili wa miradi 400 ambayo inatekelezwa na wakandarasi hapa Zanzibar.
iii. Kufanya ukaguzi wa miradi 380 ili kuhakikisha ujenzi wote unaofanyika nchini unatekelezwa kwa mujibu wa taratibu na Sheria za Bodi ya Usajili wa Wakandarasi na unatimiza viwango vya ujenzi vilivyowekwa (Standards).
iv. Kuandaa Semina, Mikutano na Mafunzo mbali mbali kwa Wakandarasi, Wadau wa Sekta ya Ujenzi, Wajumbe na Watendaji wa Bodi ili kuwajengea uwezo katika majukumu yao ya kila siku.
v. Kushajihisha wanafunzi kupenda masomo ya sayansi ili kuwa wataalamu wa fani mbali mbali katika Sekta ya Ujenzi.

**Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**108. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Bodi ya Usajili wa Wakandarasi imekadiria kukusanya Jumla ya **Shilingi 1,771,346,000** kupitia vyanzo vyake vya mapato. Asilimia 50 ya makusanyo hayo yataingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa upande wa matumizi, Bodi imepanga kutumia jumla ya **Shilingi 885, 673, 000** kwa kazi za kawaida.

## E.7 BODI YA USAJILI WASANIFU, WAHANDISI NA WAKADIRIAJI MAJENGO

**109. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Usajili, Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo ina jukumu la kusajili Wasanifu, Wahandisi, Wakadiriaji Majengo, Makampuni ya kiushauri wa kada za Usanifu, Uhandisi, Wakadiriaji Majengo pamoja na kufuatilia mwenendo wa kazi wanazozifanya na kuratibu mikutano na semina zinazohusiana na kada hizo.

**Utekelezaji wa Malengo ya Bodi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.**

**110. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

a. **Kusajili Wataalamu wa Ujenzi.** Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 , Bodi ya Usajili, Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo ilikadiria kusajili jumla ya wataalamu 95 na Makampuni ya Kishauri 14 na hadi kufikia Machi 2025, Bodi imefanikiwa kusajili jumla ya wataalamu 42 sawa na asilimia 44 ya makadirio na Makampuni ya Ushauri 13 sawa na asilimia 93 ya makadirio. Wataalamu hao ni pamoja na Washauri Elekezi wa nchini 20, Wataalamu Mahiri wa Nchini 6 na Wataalam Mahiri wa Kigeni 1, Wahitimu 13 na Fundi Sadifu wawili (2). Aidha, Kati ya Kampuni za Kishauri 13 zilizosajiliwa, Kampuni 12 za Ndani ya Nchi na Kampuni 1 ya kigeni. Kwa Ujumla Bodi ya Usajili Wasanifu Wahandisi na Wakadiriaji Majengo imeshasajili wataalamu wote waliotajwa kwenye sheria 872 na Kampuni za Ushauri 141.

b. **Usajili wa Miradi.** Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2024, Bodi ilikadiria kusajili miradi 228 na hadi kufikia Machi 2025, Bodi imefanikiwa kusajili miradi 267 sawa na asilimia 117 katika maeneo mbali mbali ya ujenzi kwa Unguja na Pemba, miradi hiyo inajumuisha Majengo ya Biashara, Nyumba za Makaazi, Hoteli, Shule, Nyumba za Ibada na mengineyo.

c. **Kufanya Ukaguzi katika Maeneo ya Ujenzi.** Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025, Bodi imekadiria kukagua miradi 190 na hadi kufikia Machi 2025, Bodi imefanikiwa kukagua miradi 109 sawa na asilimia 57.4 ya makadirio kwa Unguja na Pemba.

d. **Kutoa Elimu kwa Watendaji wa Bodi na Wadau.** Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 Bodi ya Usajili, Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo imefanikiwa kutoa elimu ya kujengea uwezo kwa kusomesha watendaji wa watano (5) kati ya sita iliyojipangia sawa na asilimia 83. Aidha, Bodi imetoa mafunzo kwa watendaji wote wa Bodi wa namna ya kutumia Mifumo ya Utendaji Kazi (MIS) ili kurahisisha utoaji huduma na kuongeza ufanisi wa kazi. Vilevile, Bodi imeendelea kutoa elimu kwa Wadau wa

Ujenzi katika kaguzi mbali mbali zinazofanywa Unguja na Pemba pamoja na kutoa matangazo yanayoelimisha jamii kuhusu usajili wa miradi ya Ujenzi.

e. **Kukuza Mashirikiano na Taasisi za Nje ya Zanzibar.** Bodi imeendelea kushirikiana kwa karibu na Bodi za Tanzania (ERB na AQRB) katika kutekeleza maeneo mbali mbali ya ushirikiano na katika muendelezo huo, watendaji wawili (2) wa Bodi wamehudhuria Mafunzo ya Uendeshaji kwa Bodi ya Uhandisi Tanzania (ERB) na Usimamizi wa Programme ya Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahitimu (SEAP programme) yenye lengo la kuwaendeleza Wahitimu Wanawake ili kukuza ushiriki wa Wahandisi Wanawake katika usimamizi wa Miradi ya Ujenzi chini ya udhamini wa Serikali ya Norway.

**Mapato na Matumizi**

**111. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Bodi ya Usajili, Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo ilikadiria kukusanya Jumla ya **Shilingi 804,000,000** na kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025 Bodi ilikadiria kukusanya Jumla ya **Shilingi 611,000,000** na hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya **Shilingi 638,071,569** zimekusanywa sawa na asilimia **104** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **79** ya makadirio ya mwaka. Asilimia **50** ya makusanyo zimeingizwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina ikiwa ni Mchango wa Bodi kwa Serikali.

Kwa upande wa matumizi, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Bodi ya Usajili, Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo ilipanga kutumia jumla ya **Shilingi 402,000,000**. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025, Bodi ilipanga kutumia jumla ya **Shilingi 313,000,000** na hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya **Shilingi 294,538,304** zimetumika sawa na asilimia **94** ya makadirio ya bajeti kwa kipindi cha miezi tisa na asilimia **73** ya makadirio ya bajeti kwa mwaka.

## MALENGO YANAYOTARAJIWA KUTEKLEZWA NA BODI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.

**112. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha, 2025/2026, Bodi ya Usajii Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuanza kutumia mifumo katika kazi za Usajili na Ukaguzi wa wataalamu ambapo imepanga kusajili wataalamu 200 wa ujenzi, kusajili miradi 400 na kukagua miradi ya ujenzi 300.
ii. Kuendelea kushajihisha Wahitimu wa Kada za Usanifu, Uhandisi na Ukadiriaji Majengo kujiunga katika Programu ya kuwaendeleza Wahitimu kwa kushirikiana na Makampuni ya Kishauri na Wakandarasi nchini pamoja na Washirika wa Maendeleo wakiwemo Serikali ya Norway, JICA na Benki ya Dunia.
iii. Kuendelea na Programu za kuwaendeleza Wataalamu wenye Kada za Usanifu, Uhandisi na Ukadiriaji Majengo na wengineo (Professional Development) kwa kutayarisha mafunzo mara mbili ya kuwaendeleza Wataalamu pamoja na kufanya Kongamano la Mwaka.
iv. Kuendelea kuimarisha uhusiano kwa kutelekeza Mpango Kazi na Taasisi zilizoingia Mkataba wa Mashirikiano (MoU) na Bodi ambazo ni IAESZ ya Zanzibar na AQRB, ERB za Tanzania pamoja na kuanzisha mashirikiano ya Taasisi zilizopo katika EAC na Duniani kwa Ujumla.
v. Kuwajengea uwezo watendaji 10 wa Bodi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi katika fani tofauti.

### Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**113. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026, Bodi ya Wasanifu Wahandisi na Wakadiriaji Majengo imekadiria kukusanya Jumla ya **Shilingi 1,670,000,000** na kutumia Jumla ya **Shilingi 830,000,000** kwa kazi za kawaida. Asilimia **50** ya makusanyo yataingizwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

## E.8. SHIRIKA LA MAWASILIANO (ZICTIA)

**114. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA) limeanzishwa kwa Sheria nambari 4 ya Mwaka 2023 na limepewa jukumu la kusimamia na kuendesha Miundombinu ya Kimkakati ya Mawasiliano ambayo ni Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano wa Zanzibar na Kituo cha Taifa cha Kuhifadhia Taarifa (Data Center).

**Utekelezaji wa Malengo ya Shirika kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.**

**115. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 ZICTIA imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo: -

a. **Kuunganisha Vituo vya Taasisi za Serikali na Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano:** Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025 ZICTIA imefanikiwa kuviunganisha na Mkonga jumla ya Vituo kumi na tisa (19) vya Taasisi mbalimbali Unguja na Pemba ikiwemo Shirika la Bima Zanzibar – Airport, Ofisi ya Rais Migombani, Nyumba ya Mapumziko (Rest House) – Maisara, Adela ZanNet (Pongwe na Kendwa), Ofisi ya CCM Mbuyu Mnene, Maegesho ya Magari – Malindi, Nyumba ya Mheshimiwa Spika – Migomabni, Ofisi za Usalama mazizini, mbweni na Chukwani kwa upande wa Unguja.

   Kwa upande wa Pemba ni Wakala wa Uchapaji – Chake chake, Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar kilichopo – Kituo cha Afya Mzambarau Takao, Shirika la Nyumba – Mkoani, Kitengo cha Ukimwi – Machomane, Ofisi ya Mkemia Mkuu – Madungu, Shirika la Umeme – Wete, Tibirinzi, pamoja na Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi – Wete.

b. **Kufikisha Huduma ya e- learning:** ZICTIA ilipanga kufikisha huduma ya e- learning kupitia (Server) ambazo zitawekwa katika Ofisi ya Shirika na Kampuni ya Dolphin, ili kufanikisha lengo hili. ZICTIA imeanza kazi ya kuziunganisha na Mkonga jumla ya Skuli mia moja (100) Unguja na Pemba ambapo kwa sasa jumla ya

Skuli zilizokwisha kupatiwa huduma ya kuunganishwa na Mkonga ni Arobaini na Tisa (49) Unguja na (26) Pemba ikiwa ni sawa na Asilimia 55 ya utekelezaji wa kazi hiyo.

Kwa upande wa Pemba, Skuli zilizokwisha fikishiwa huduma hii ni:- Skuli ya Sekondari Ole, Uwandani, Kituo cha Walimu (TC) Michakaeni, Fidel Castro, Konde, Mchangamdogo, Hemed Suleiman, Pujini hub, Gando, Mkote, Wete, Utaani, Chasasa, Limbani, Kizimbani, Mbuzini, Pondeani, Wesha, Shamiani, Wingwi, Kituo cha Walimu (TC) Wingwi, Maktaba Chake, Minungwini pamoja na Skuli ya Msingi Ole na Michakaeni.

Kwa Upande wa Unguja, Skuli zilizokwisha fikishiwa huduma hii ni:- Skuli za Sekondari Mkokotoni, Donge, Chukwani, Bubwini, Mgambo, Mfenesini, Kijini, Mbuzini, Mpendae, Muungano, Ali Hassan Mwinyi, Mikindani, Mtoni Kidatu, Chwaka, Mikunguni, Mkwajuni, Tumekuja, Muwanda, Kijichi, Mahonda, Munduli, Mwera, Donge Mchangani, Regeza Mwendo pamoja na Skuli ya Msingi Donge. Aidha, Vituo vya Walimu vilivyofikishiwa huduma ni pamoja na Bwejuu, Unguja Ukuu, Hasnuu Makame, Kisauni, Mkwajuni, Mahonda Muwanda, Bububu, Uroa, Dunga, Mbadala, Kitope, Chuini, Jang'ombe, Mtoni Kigomani, Chumbuni, Maungani, Jumbi, Fuoni Rock, Kizimkazi Mkunguni na Makunduchi.

c. **Maboresho ya Mkonga wa Mawasiliano:** Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025, ZICTIA imeendelea na maboresho ya Mkonga katika maeneo mbalimbali yenye urefu wa kilomita 309 Unguja na Pemba. Kwa upande wa Unguja, kazi hiyo imefanyika katika maeneo ya Upenja, Donge Skuli, Mahkama ya Vuga, Uzi, Tomondo, Garagara, Mwanakwerekwe - Kijitoupele, Darajani Souk, Paje, Michamvi, Kisiwandui, Mazizini – Chukwani, Mazizini – Mnazimmoja, Mazizini – Kisauni, Masingini – Dole, Mazizini – Mwanakwerekwe, Mtoni Kidatu, Mazizini – K/Samaki, na Paje – Makunduchi, Kitogani – Kibuteni, Kibuteni – Kizimkazi, Kibuteni – Makunduchi, Jumbi

– Mwera Pongwe, Chwaka – Uroa, Matemwe Muyuni, Mkapa road – Kinazini pamoja na Mazizini - Amani.

Kwa upande wa Pemba, kazi ya uboreshaji wa Mkonga imefanyika katika maeneo ya Hospitali ya Abdalla mzee, Wete - Utaani, Chamanangwe, Mkoani, Micheweni, Finya, Bahanasa, Kinyasini na Mchangamdogo. Aidha, kazi ya uimarishaji wa huduma katika vituo vya kupokelea na kurushia mawasiliano (PoP) kwa kuvifanyia maboresho (services) Vipoza hewa (AC) na Majenereta imeendelea katika Vituo vyote kumi na mbili (12) vya Unguja na Pemba.

d. **Kuhifadhi Taarifa za Mifumo katika Kituo cha Kuhifadhia Taarifa (Data Center):** Katika kipindi cha Julai 2024, hadi Machi, 2025 ZICTIA imeendelea kupokea na kuihifadhi katika Kituo cha Kuhifadhia Taarifa (Data Centre) jumla ya mifumo mipya Ishirini na Tatu (23) kutoka katika taasisi (9) mbali mbali za Serikali. Taasisi hizo ni pamoja na Shirika La Nyumba Zanzibar, Wizara Ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Ofisi ya Makamo Wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Taasisi ya Ziaat, Wakala Wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Taasisi ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar – Zaeca na Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar.

e. **Uunganishaji wa Mkonga wa Taifa na Minara.** Wizara kupitia ZICTIA imeafanikiwa kutekeleza Mradi wa uunganishaji wa Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano Minara 130 ya Kampuni ya Honora (Yas) sawa na jumla ya kilomita 148 za Mkonga uliosambazwa. Lengo ni kuondosha changamoto za mawasiliano kwa wananchi katika maeneo mbali mbali Zanzibar.

f. **Upelekaji wa Mkonga Majumbani;** Wizara kupitia ZICTIA imeendelea na mchakato wa utekelezaji wa kupeleka huduma nafuu ya matumizi ya TEHAMA kwa kuufikisha

Mkonga majumbani (Fiber To The Home - FTTH), Mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya ZICTIA na HONORA (YAS) ambapo kwa sasa taratibu za kuandaa Mkataba Mkuu zinaendelea ili kuanza rasmi utekelezaji wa mradi huo.

g. **Mradi wa Uanzishaji wa Mji wa Kidijitali,** Wizara kupitia ZICTIA imefanikiwa kuanza utekelezaji wa Mradi wa Uanzishaji wa Zanzibar ya Kidjitali (Zanzibar Digital Initiatives) unaojumuisha upembuzi yakinifu juu ya uandaaji wa Mpango Mkuu wa Mji wa Kidijitali Zanzibar (Master Plan for the Zanzibar Cyber City), uandaaji wa Mkakati wa Maendeleo ya Ujuzi wa Kidijitali na kuanzishwa kwa Taasisi ya Ujuzi wa Kidijitali Zanzibar (The Development of Zanzibar Digital Skills Development Strategy and the establishment of the Digital Skills Institute in Zanzibar) na uanzishwaji wa Kituo cha Taifa cha Ubunifu na Mfuko wa Taifa wa Ubunifu (The Study on Creating a Zanzibar National Innovation Hub and Fund). Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania .

h. **Kuwapatia Mafunzo Watendaji wa ZICTIA:** Katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2024-2025 jumla ya wafanyakazi kumi na tatu (13) walihudhuria mafunzo ya muda mfupi katika vyuo mbali mbali nchini kwa lengo la kuwaongezea ufanisi katika maeneo yao ya kazi, ambapo wafanyakazi wawili (2) kati ya hao wameshiriki katika Mkutano wa Kumi na Mbili (12) wa Chama cha Menejimenti ya Kumbukumbu na Nyaraka Tanzania (TRAMPA), mmoja (1) alishiriki Mkutano wa Tisa (9) wa Mtandao wa Wasimamizi na Mameneja wa Rasilimali watu katika Sekta za Umma Barani Afrika, wawili (2) wameshiriki katika mafunzo ya Data Management ambayo yalitolewa na Digital for Tanzania Project (DTP), mmoja (1) alishiriki katika mafunzo ya uandaaji wa Bajeti

za Taasisi za Umma, mmoja (1) ameshiriki mafunzo juu ya uandaaji wa udhibiti wa taarifa za fedha za ndani ambapo mwengine ameshiriki katika Jukwaa la 11 la Uongozi. Vile vile, wafanyakazi (2) wamejifunza stadi za upulizaji wa madawa katika majengo, wawili (2) wameshiriki katika Kongamano la tatu la Kitaalamu la Chama cha Madereva wa Serikali Tanzania na mmoja (1) ameshiriki mafunzo juu ya Utayarishaji wa Taarifa za Fedha kwa kutumia viwango vya Kimataifa vinavyozingatia Sekta ya Umma. Aidha, wafanyakazi wote wamepatiwa mafunzo ya elimu mtambuka yanayohusiana na maradhi yanayoambukiza na yasiyoambukiza ikiwemo Ukimwi, Kisukari na Homa ya Inni B na C katika Maadhimisho ya Wiki ya Mashirika ya Umma Zanzibar.

**Mapato na Matumizi**

**116. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha, 2024/2025, Shirika la Mawasiliano Zanzibar lilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 15,877,471,996** na kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 ilikadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 11,691,853,997** kupitia vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya **Shilingi 11,986,686,119.69** zimekusanywa sawa na asilimia **102** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **75** ya makadirio ya mwaka.

**117. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Shirika la Mawasiliano Zanzibar lilipangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 15,949,359,616**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,074,798,800** ni mishahara, **Shilingi 5,874,560,816** ni kazi za kawaida na **Shilingi 8,000,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025 ilipanga kutumia jumla ya **Shilingi 13,162,589,916** na hadi kufikia Machi 2025, jumla ya **Shilingi 8,650,994,880.90** zimetumika sawa na asilimia **65.7** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **54** ya mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,294,614,709**

ni mishahara, **Shilingi 6,022,492,009.68** kwa kazi za kawaida na **Shilingi 1,333,888,161.94** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**MALENGO YA SHIRIKA LA MAWASILIANO (ZICTIA) YANAYOTARAJIWA KUTEKLEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**.

**118. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Shirika la Mawasiliano Zanzibar limepanga kutekeleza miradi ifuatayo: -

i. Kuanza Ujenzi wa Kituo Mbadala cha Kuhifadhia Taarifa (Data Center) katika Maeneo ya uwekezaji Fumba ambapo kazi ya Upembuzi yakinifu tayari imekamilika.
ii. Kuanza Mradi wa kulaza Mkonga wa Baharini "International Gateway" kutoka Mombasa, Kenya - Micheweni, Pemba - Fumba, Unguja. Hii itasaidia katika kukuza uchumi wa nchi kupitia upatikanaji wa huduma ya mtandao (Internet) kwa Serikali na Sekta Binafsi ndani ya Zanzibar ambapo kazi ya Upembuzi Yakinifu imekamilika.
iii. Uimarishaji wa Mfumo wa Mawasiliano kwa lengo la kuendelea kufanya matengenezo yanayotokana na Mkonga unaoharibika kutokana na ujenzi wa barabara mbalimbali zinazojengwa nchini.
iv. Ujenzi wa Kituo Mbadala cha Kuhifadhia Taarifa - Pemba (Data Recovery Site). Ujenzi wa kituo hicho kutasaidia kuhifadhi taarifa endapo kutajitokeza tatizo litakalosababisha kupotea kwa taarifa.
v. Mradi wa Umarishaji wa Vifaa vya Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano. Lengo la Mradi ni kuongeza uwezo wa matumizi ya Mkonga ili kukuza uchumi wa kidijitali Zanzibar.
vi. Kuendelea kuzifanyia matengenezo kilomita 350 za Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano Unguja na Pemba.

vii. Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi wafanyakazi 20 katika fani tofauti ili kuimarisha utendaji wao.

**Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**119. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Shirika la Mawasiliano (ZICTIA) Zanzibar limekadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 16,091,598,760** kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato.

Kwa upande wa matumizi, Shirika limepanga kutumia jumla ya **Shilingi 12,559,155,871** kwa kazi za kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,193,397,200** ni mishahara, **Shilingi 5,365,758,671** matumizi mengineyo na **Shilingi 5,000,000,000** kwa ajili ya kazi ya mradi wa maendeleo.

## F. MASHIRIKIANO NA TAASISI ZA MUUNGANO

**120. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imeendelea kushirikiana na Taasisi za Muungano zilizopo hapa Zanzibar katika utoaji wa huduma na usimamizi wa Sekta ya Mawasiliano na Uchukuzi. Miongoni mwa Taasisi hizo ni Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Tanzania (TCAA), Mamlaka ya Hali ya Hewa ya Tanzania (TMA), Mamlaka ya Mawasiliano ya Tanzania (TCRA), Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Shirika la Huduma za Posta Tanzania (TPC), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC).

**121. Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kushirikiana kwa karibu na Wizara zisizokuwa za Muungano za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo zinashabihiana kimajukumu kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma katika Sekta ya Uchukuzi, Ujenzi na Mawasiliano hapa Zanzibar. Wizara hizo ni:- Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mashirikiano na Wizara hizi pamoja na Taasisi zake yamechangia sana kukuza Sekta za Ujenzi, Sekta ya Uchukuzi na Sekta ya Mawasiliano hapa Zanzibar.

Napenda kuchukua nafasi hii kuzipongeza Wizara hizo na Taasisi zake kwa kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na nachukua fursa hii kuzitaka ziendeleze ushirikiano huo kwa maslahi mapana ya Nchi yetu.

## G. MCHANGO WA SEKTA BINAFSI KATIKA KUIMARISHA SEKTA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO.

**122. Mheshimiwa Spika,** Sekta Binafsi imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kusaidia juhudi za Serikali za kuendeleza na kuimarisha huduma za Ujenzi na Majengo, kuimarisha huduma za Usafiri wa Anga, Baharini na Nchi Kavu (Barabara) pamoja na huduma za Mawasiliano hapa Zanzibar. Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi inatambua na kuthamini mchango wa Sekta binafsi katika kujenga uchumi wa Nchi yetu kwa kutoa huduma bora zenye kufanikisha sekta nyengine za kiuchumi na kijamii, kuchangia Pato la Taifa na kutoa ajira kwa wananchi. Wizara itaendelea kuhamasisha na kuweka mazingira mazuri ya kisera kwa sekta hizo ili ziendelee kuimarisha huduma za Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano hapa Zanzibar.

**123. Mheshimiwa Spika,** Nakuchukua nafasi hii kuzipongeza Taasisi Binafsi zinazotoa huduma mbalimbali za Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano kwa kazi nzuri wanayoifanya na naziomba ziendelee kushirikiana na Serikali katika kuwahudumia wananchi. Aidha, nizipongeze Kampuni ya DNATA, Kampuni ya SEGAP, Kampuni ya Emirate leisure. Kampuni ya ZMT, Fumba Port, Kampuni ya ZF Devco, Kampuni ya ZENJI Machandise, Kampuni ya Ndani Investment Cooparation, Kampuni ya Vodacom na Kampuni ya Yas kwa ushirikiano na mchango wao kubwa wanaoutoa kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na kuhakikisha kuwa huduma za Usafiri wa Anga, huduma za Usafiri Baharini, huduma za Usafiri wa Barabara pamoja na huduma za Mawasiliano zinakuwa bora na zenye ufanisi hapa Zanzibar.

## H. MUELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI KWA KILA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

124. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji kwa kila Programu zinazosimamiwa na Wizara pamoja na Taasisi zinazojitegemea zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, kwa ruhusa yako sasa, naomba kuwasilisha muelekeo wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

### H.1. VIPAUMBELE VIKUU VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

125. **Mheshimiwa Spika,** Matayarisho ya Bajeti hii yamezingatia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (2050), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030, Sera ya Taifa ya Usafiri Zanzibar (2008), Sera ya TEHAMA (2013), Mpango Mkuu wa Usafiri Zanzibar (Zanzibar Transport Master Plan - 2007), Mpango wa Taifa wa Maendeleo Zanzibar - ZADEP (2021-2026), Sera mbalimbali za sekta mtambuka za Taifa, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020-2025), Mpango Mkakati wa Wizara (Strategic Plan), Takwimu za matokeo ya Sensa ya Watu na Makaazi ya Mwaka 2022, Ahadi na Maagizo mbalimbali yaliyotolewa na Viongozi Wakuu wa Kitaifa pamoja na maandalizi ya mashindano ya Mpira wa Miguu wa Mataifa ya Afrika (AfCON inayotarajiwa kufanyika mwaka 2027 ambayo Tanzania itakuwa miongoni mwa Nchi zitakazoandaa mashindano hayo (Host Country).

126. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia Miongozo hiyo pamoja na Ahadi na Maagizo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa wa Nchi, katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026, Vipaumbele vikuu vya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ni :- Kuendelea kuimarisha Miundombinu ya Bandari, Miundombinu ya Usafiri wa

Barabara, Miundombinu ya Usafiri wa Anga, Miundombinu ya Mawasiliano ili kufikia uchumi wa kidijitali, kuimarisha Miundombinu ya Kuondolea maji ya mvua ndani ya mji wa Zanzibar, kutayarisha Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali itakayowezesha kusimamia na kutoa huduma bora kwa jamii katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi hapa Zanzibar.

## H.2 MUHTASARI WA MAELEZO KWA KILA PROGRAMU NA MALENGO YANAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**127. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Programu Kuu nne (4) ambazo ni: - Programu ya Usafirishaji, Programu ya Ujenzi na Majengo, Programu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) pamoja na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

**128. Mheshimiwa Spika,** Programu kuu zilizoainishwa katika Bajeti hii zimewekewa malengo makhususi, matokeo ya muda mrefu yatakayopatikana, huduma zitakazotolewa, Shabaha na Viashiria mbalimbali vitakavyotumika kupima utekelezaji wa Huduma zitakazotolewa kupitia Sekta Ujenzi, Sekta ya Mawasiliano na Sekta ya Uchukuzi. Maelezo ya Programu hizo ni kama ifuatavyo:-

## PP0101 - PROGRAMU YA USAFIRISHAJI.

**129. Mheshimiwa Spika,** Matokeo yanayotarajiwa kupatikana katika Programu hii ni kuwepo kwa miundombinu na huduma za usafiri zilizo bora, salama na endelevu. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu ya Usafirishaji itakuwa na Programu Ndogo moja ambayo ni; Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji.

## SP010101 - Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji

**130. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Wakala wa Barabara Zanzibar na Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar. Programu hii ina lengo la kuhakikisha huduma bora za usafiri zilizo salama zinapatikana muda wote Unguja na Pemba. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara kupitia Taasisi zinazosimamia Programu hii, imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

## IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

**131. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji imepanga kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ifuatayo: -

i. Kuendelea na Ujenzi wa Barabara kuu Unguja na Pemba; miongoni mwa Barabara zinazoendelea na zitakazoanza kujengwa kwa upande wa Unguja ni:- Barabara ya Tunguu – Makunduchi 48 km , Fumba – Kisauni 12 km, Kitogani – Paje, Barabara ya Bumbwini – Pangatupu - Mahonda 11.3km, barabara ya Mangapwani – Zingwezingwe – Mahonda 8.4km, Barabara ya Mfenesini – Mangapwani 7.2km, Barabara ya Nungwi – Muyuni 13km, Mkwajuni – Matemwe km 7.4, Mkwajuni – Kijini km 9.2, Kizimkazi – Makunduchi 14.18km, Barabara ya Mahonda – Donge – Mkokotoni 13.1km, Barabara ya Paje – Michamvi 18km, Barabara ya Mtoni – Bububu 4km, Kianga - Istiqama 3km, Barabara Mbuzini - Kijichi 6km, Barabara ya Ubago - Jumbi 6.5km, Barabara ya Langoni - Kwabiasha km4.5 na barabara ya Uzi – Ng’ambwa pamoja na Daraja kilomita 8.7.

   Kwa upande wa Pemba ni: - Barabara ya Chake – Mkoani 43.5 km, Barabara ya Gando – Wete – Konde km 26.5, Barabara ya Mtambile – Kengeja 10 km, Barabara Goli la

Mpira - kwa Popo 4.2km, Barabara ya Mihogoni - Uhanda - Amani 2.2km , Barabara ya Pujini Skuli - Chuo cha Mwalimu Nyerere 2.6 km, Barabara ya Chwale – Kilindini – Konde 24 km, Barabara ya Micheweni – Kilindini 5.4 km, Barabara ya Machomanne – Wawi - Vitongoji 8 km, barabara ya Chake – Wesha 7.4 km, Barabara ya Kianga – Gombani 6 km, Barabara ya Chanjamjawiri – Tundauwa km 10.7 pamoja na kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Chake - Wete 22.1km. Baadhi ya barabara hizo, zinazoendelea na zitakazojengwa zinaonekana katika **kiambatanisho Nambari 4 na 5.** Kwa ujumla ujenzi wa Barabara Kuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 umetengewa kutumia jumla ya **Shilingi 256,531,867,000.**

ii. Kuendelea kukamilisha ujenzi wa Barabara za ndani zenye urefu wa Kilomita 275.9 Unguja na Pemba. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 78,034,000,000.**

iii. Kukamilisha Ujenzi wa barabara za Mjini Unguja zenye urefu wa kilomita 100.9 Awamu ya kwanza. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 35,000,000,000**.

iv. Kuendelea na ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba kwa kuongeza urefu wa Barabara ya Kutulia na Kurukia Ndege, Njia ya Kupitia Ndege pamoja na Maegesho ya Ndege (Runway, Taxi way and Apron), kujenga Jengo Jipya la Abiria (Terminal Building) na miundombinu husika itakayowezesha uwanja huo kutua ndege aina ya Code C (Boeing 737-800) na zinazolingana. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 234,000,000,000**.

v. Kukamilisha ujenzi wa Jengo la Abiria Terminal II Awamu ya Kwanza, kuanza ujenzi wa Jengo la Abiria Terminal II Awamu ya Pili pamoja na kujenga Jengo Jipya la Kuongozea Ndege (Control Tower) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa AAKIA. Kwa Mwaka wa Fedha

2025/2026, Mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 60,000,000,000.**

vi. Kuanza ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Nungwi ili uweze kutoa huduma kulingana na Viwango vya Kimataifa. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mradi huu umepangiwa kutumia Jumla ya **Shilingi 22,500,000,000**.

vii. Kuanza ujenzi wa Maegesho ya Ndege (Apron) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Kurume. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mradi huu umepangiwa kutumia Jumla ya **Shilingi 40,000,000,000**.

viii. Kuendelea na ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani, kuweka miundombinu katika eneo la bandari pamoja na kukamilisha nyumba za fidia katika eneo la Mangapwani. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mradi huu umepangiwa kutumia Jumla ya **Shilingi 205,100,364,000**.

ix. Kujenga Bandari mpya ya Kisasa ya Abiria katika eneo la Maruhubi. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 130,000,000,000**.

x. Kuanza Mradi wa Uwekaji wa Kamera za Kisasa za Kusimamia Usafiri Barabarani (Smart Traffic Camera) ili kuimarisha usalama kwa Watumiaji wa Barabara pamoja na kubaini makosa yanatokana na uvunjifu wa Sheria na Kanuni za Usalama Barabarani. Kwa Mwaka Fedha, 2025/2026 Mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 1,873,000,000**.

xi. Kukamilisha Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usafiri wa Umma Zanzibar ambao unahusisha utafiti utakaotoa mwelekeo wa namna ya kuimarisha usafiri huo. Mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 374,338,000.**

**132. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu ndogo

ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji imepanga kutumia jumla ya **Shilingi 1,063,413,569,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo Unguja na Pemba, ikiwa **Shilingi 485,513,249,000** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na **Shilingi 577,900,320,000** zitatolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR

**133.Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wakala wa Barabara Zanzibar kupitia Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji imepanga kuzifanyia matengenezo barabara mbalimbali Unguja na Pemba kama ifuatavyo:-

i. Kujenga barabara za ndani Mchangani 1.3km, barabara ya Mshelishelini – Bandamaji 2.15 km, barabara ya Chuini – Mawimbini 1.5 km, barabara ya mzunguko ya Uchukuni (kiboje) km 4.5 na barabara ya Kisakasaka Machinjioni 1.3 km.

ii. Kujenga njia za waendao kwa miguu na uwekaji wa taa za barabarani aina ya solar kwa barabara za ndani za kizimkazi 2.6 km.

iii. Kukamilisha ujenzi wa barabara ya Mgelema – Wambaa 4.1 km, Msihakwe – Kipapo – Mgelema 0.35 km na barabara Kinyasini – Hospital ya Wilaya ya Wete 0.7 km.

iv. Kujenga barabara ya Wawi – Mwanzo Mgumu 2 km, Barabara ya Chumbageni – Tondooni 2.2 km, barabara ya Mauwani –Kirimdomo 1km, barabara ya Pujini School – Mkamandume – Kibaridi – Bandarini 2.5 km na barabara ya Pandani – Mlindo 3.2km.

v. Kuendelea kuzifanyia matengenezo ya kawaida barabara za lami Unguja na Pemba.

vi. Kuweka michoro na alama za barabarani kwa barabara mbalimbali Unguja na Pemba ili kuimarisha usalama kwa watumiaji wa barabara hizo.

vii. Kuendelea kutoa huduma ushauri Elekezi kwa baadhi ya miradi ya barabara inayojengwa na Wakandarasi.

viii. Wakala wa Barabara itaendelea kutekeleza shughuli za kiutumishi na utawala kwa kununua vifaa mbalimbali vya Ofisi pamoja na kuweka mazingira mazuri ya kazi.

ix. Kuwajengea uwezo wafanyakazi 40 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi.

**134. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wakala wa Barabara Zanzibar imepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 25,853,200,000** ikiwa ni Ruzuku kutoka Serikalini kwa kazi za kawaida na matengenezo ya Barabara Unguja na Pemba. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 6,240,000,000** ni mshahara, **Shilingi 968,774,000** ni matumizi mengineyo, na **Shilingi 18,644,426,000** ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

## WAKALA WA KARAKANA KUU YA MAGARI ZANZIBAR

**135. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar kupitia Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji imepanga kutekeleza yafuatayo: -

i. Kuziimarisha Karakana za Serikali kupitia Ubiya na Kampuni Binafsi (PPP) ili kuongeza uwezo wa kutoa huduma kwa kufanya matengenezo ya magari hadi kufikia 2,700 Unguja na Pemba.

ii. Kuendelea kutoa Ushauri wa kitaalamu wa ununuzi na uuzaji wa magari hadi kufikia taasisi 50.

iii. Kuimarisha huduma za utawala na utumishi ikiwemo kununua vifaa mbalimbali vya ofisi pamoja na kusimamia maslahi ya watumishi wa Taasisi.

iv. Kuwajengea uwezo Wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu Wafanyakazi 6 na mafunzo ya muda mfupi Wafanyakazi 13 Unguja na Pemba.

v. Kuandaa Sheria mpya ya Wakala wa Karakana Kuu ya Magari ili iweze kutoa huduma bora zitakazopelekea kuongezeka vyanzo vipya vya mapato.

vi. Kufanya ukarabati wa miundombinu ya kiufundi katika Karakana za Wakala ikiwemo kubadilisha teknolojia za kiufundi ili kuendana na wakati.

vii. Kuandaa mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kurahisisha utoaji na upatikanaji wa huduma na taarifa zinazohusiana na Wakala.

136. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha, 2025/2026 Wakala wa Karakana Kuu ya Magari imepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 2,873,000,000** ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,531,800,000** ni mshahara na **Shilingi 1,341,200,000** ni matumizi mengineyo.

137. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji inaombewa kutumia jumla ya **Shilingi 1,092,298,979,000** kwa kazi za kawaida, ruzuku na miradi ya maendeleo kwa taasisi zinazosimamia Programu hii.

## PP0105 - PROGRAMU YA UJENZI NA MAJENGO

138. **Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya Programu hii ni kuwepo kwa usimamizi imara wa ujenzi na majengo bora ya Serikali na binafsi yaliyo salama na yenye viwango vinavyokubalika kwa mujibu wa miongozo iliyopo na yenye kukidhi mahitaji ya watumiaji wote. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 programu hii itakuwa na Programu ndogo moja ambayo ni; Usimamizi wa Ujenzi na Majengo.

### SP010501 - Programu ndogo ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo.

139. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara

ya Mipango, Sera na Utafiti pamoja na Wakala wa Majengo Zanzibar na ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa usimamizi imara wa ujenzi wa miundombinu na majengo bora ya Serikali na binafsi yaliyo salama. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara kupitia Taasisi zinazosimamia Programu hii, imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

## IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

**140. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia programu ya Ndogo ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo imepanga kusimamia utekelezaji wa miradi na kazi zifuatazo:-

i. Kuanza ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua na mabwawa ya kuhifadhia maji ya mvua katika mji wa Zanzibar. Mradi huu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 umepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 270,000,000,000**.

ii. Kuimarisha miundombinu mbalimbali itakayosaidia kukuza uchumi katika miji ya Unguja na Pemba ikiwemo Mji wa Mkoani, Micheweni, Wete na Chake, Maeneo ya Sebleni – Kwawazee na Magomeni pamoja na ujenzi wa bwawa la Mwantenga na Ziwa Maboga. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 140,000,000,000**.

**141. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu Ndogo ya Usimamizi wa ujenzi na majengo imepanga kutumia jumla ya **Shilingi 410,150,730,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kazi za kawaida kwa Unguja na Pemba, ikiwa **Shilingi 140,000,000,000** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, **Shilingi 270,000,000,000** ni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na **Shilingi 150,730,000** ni matumizi mengineyo.

**WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR**

**142.Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wakala wa Majengo kupitia Programu Ndogo ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea kutoa huduma za Ushauri Elekezi kwa miradi mbali mbali ya ujenzi wa majengo ya Serikali.

ii. Kuandaa Nyaraka za ujenzi na BoQ 39, kati ya Nyaraka hizo, 24 zitaandaliwa kwa upande Unguja na 15 zitaandaliwa kwa upande Pemba.

iii. Kufanya mapitio ya Nyaraka za ujenzi na BoQ 12 kwa Nyaraka ambazo hazijaandaliwa na Wakala wa Majengo.

iv. Kusimamia Miradi 47 ya ujenzi, kati ya Miradi hiyo 32 itasimamiwa Unguja na 15 itasimamiwa Pemba.

v. Wakala wa Majengo kwa kushirikina na Wizara imepanga kukamilisha mchakato wa uandaaji wa Sheria ya Wakala wa Majengo Zanzibar.

vi. Kujenga Jengo la Afisi za Wakala wa Majengo ili kuwa na afisi za kudumu kwa lengo la kuweka mazingira mazuri na kuongeza ufanisi kwa kazi za kila siku.

**143. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha, 2025/2026 Wakala wa Majengo imepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 3,040,700,000** ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 2,065,700,000** ni mishahara na **Shilingi 975,000,000** ni matumizi mengineyo.

**144. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Ujenzi na Majengo inaombewa kutumia jumla ya **Shilingi 413,191,430,000** kwa miradi ya maendeleo, kazi za kawaida na ruzuku kwa Taasisi zinazosimamia Programu hii.

**PP0103 - PROGRAMU YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA).**

**145.Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya Programu hii ni kuwepo kwa miundombinu na huduma bora na salama za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Programu hii ina Programu Ndogo moja ambayo ni Miundombinu na Huduma za TEHAMA.

**SP010301 - Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA.**

**146.Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara ya Mawasiliano na ina lengo la kusimamia uwepo wa miundombinu na huduma bora za TEHAMA zilizo salama na endelevu pamoja na kushajihisha Ubunifu na Uchumi wa Kidijitali kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji yanayotokana na uwekaji wa Sera na Sheria rafiki.

**147. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Idara ya Mawasiliano kupitia Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA ili kufikia Uchumi wa Kidijital imepanga kusimamia utekelezaji wa Miradi na kazi zifuatazo:-

i. Kuendelea kuimarisha Mifumo ya Mawasiliano Zanzibar kwa kuimarisha Miundombinu ya Mkonga pamoja na kutengeneza mifumo mbalimbali ya kidijitali ikiwemo Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Taasisi zote za Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, mfumo wa usimamizi wa Fidia kwa Wizara, Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Miradi ya Wizara, Kuandaa "Masterplan ya Cyber City "pamoja na kuweka anuani mpya za majengo 5,000. Mradi huu kwa Mwaka wa Fedha, 2025/2026 umepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 6,000,000,000**.

ii. Kuanza mradi wa kulaza Mkonga wa Kimataifa baharini "International Gateway" kutoka Mombasa, Kenya hadi Micheweni, Pemba kuelekea Fumba, Unguja. Mradi huu kwa Mwaka wa Fedha, 2025/2026 umepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 30,000,900,000.**

iii. Kuanza ujenzi wa Kituo Mbadala cha Kuhifadhia Taarifa (Data Center) katika maeneo ya uwekezaji Fumba. Mradi huu kwa Mwaka wa Fedha, 2025/2026 umepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 30,000,000,000**.

iv. Kuimarisha huduma za mtandao katika maeneo ya umma (Public Wi-Fi) (Amani, Nyamanzi na Kijangwani). Mradi huu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 umepangiwa kutumia jumla ya **Shilingi 10,050,000,000**.

Aidha, kazi nyengine ambazo Idara ya Mawasiliano imepanga kutekeleza ni:-

v. Kutayarisha Miongozo ya Mageuzi ya Kidijitali Zanzibar pamoja na kukamilisha Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Faragha (PDPC) na Wabunifu Chipukizi (Startups).

vi. Kuweka mazingira wezeshi kwa kuimarisha Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na kuvutia Wawekezaji kwa kuweka Sera, Sheria na Kanuni ambazo zinaendana Kitaifa na Kimataifa.

vii. Kuboresha Mfumo wa Anuani za Makaazi Zanzibar pamoja na kuwapatia Wananchi uelewa wa matumizi ya Mfumo huo.

viii. Kuendelea kuwajengea uwezo wananchi 2,500 kwa kuwapatia mafunzo ya kidigitali kupitia vituo vya TEHAMA jamii, kuboresha na kuanzisha Vituo vipya katika maeneo tofauti.

ix. Kujenga na kusimamia Kituo cha Ubunifu na Ujasiriamali (Digital Innovation and Enterprenuership) katika Sekta ya TEHAMA kwa lengo la kuwajengea uwezo vijana, kuibua vipaji na kuongeza Soko la Ajira kupitia TEHAMA

x. Kujenga uelewa wa matumizi ya TEHAMA kwa makundi maalumu na wenye mahitaji maalumu.

148. **Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza malengo haya, Wizara kupitia Idara ya Mawasiliano, imejipanga kuchukua hatua za msingi za kushirikiana na wadau wa maendeleo katika Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ili kupata nguvu ya pamoja ya kutekeleza malengo ya maendeleo

endelevu ya Mwaka 2030. Pia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya Mwaka 2050 imeainisha na kutoa kipaumbele kwa Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuwa ndio Sekta wezeshi kufikia malengo ya Dira hiyo ya Uchumi wa Kidijitali.

149. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA inaombewa kutumia jumla ya **Shilingi 76,973,814,000** kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 379,914,000** ni mishahara, **Shilingi 543,000,000** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 76,050,900,000** kwa ajili ya kazi za maendeleo.

## PP0104 - PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA

150. **Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya Programu hii ni kuwepo kwa uratibu wa Shughuli za Wizara, Sera, Mipango ya Kisekta pamoja na usimamizi mzuri wa rasilimali watu. Programu hii ina Programu Ndogo tatu (3) ambazo ni; Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara pamoja na Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba.

### SP010401 - Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji

151. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi na ina lengo la kuimarisha huduma za ofisi na usimamizi wa rasilimali watu katika Wizara.

152. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Idara ya Uendeshaji na Utumishi kupitia Programu hii itaendelea kutekeleza yafuatayo: -

   i. Kuendelea kusimamia masuala ya kiutumishi na uendeshaji wa Wizara ikiwemo kuweka mazingira mazuri ya kazi, kusimamia maslahi ya watumishi na kuwapatia vitendea kazi ili kuongeza ufanisi wa kazi pamoja na kuvifanyia matengenezo vyombo vya usafiri.

ii. Kutoa Makala na Machapisho mbalimbali kuhusu utekelezaji wa shughuli na mafanikio ya Wizara pamoja na kuratibu safari za kikazi za ndani ya nchi na nje ya nchi.

iii. Kuwajengea uwezo watendaji ili kuongezea ujuzi, ufanisi na tija kwa wafanyakazi wa Wizara Unguja na Pemba kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa mujibu wa Mpango wa Mafunzo wa Wizara.

**153. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji inaombewa kutumia jumla ya **Shilingi 4,463,128,000** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,313,128,000** ni mshahara na **Shilingi 2,150,000,000** ni matumizi mengineyo.

**SP010402 - Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara**

**154. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na ina lengo la kuhakikisha Mipango na Sera mbalimbali katika Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi zinatayarishwa pamoja na kufuatilia utekelezaji wake.

**155. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na kufuatilia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

ii. Kutayarisha Muongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Utekelezaji wa Kazi za Wizara.

iii. Kutoa mafunzo ya utayarishaji wa bajeti kwa watendaji wa Wizara kulingana na Miongozo kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango inayotolewa kila Mwaka.

iv. Kuratibu na kufanya tafiti zinazohusu Sekta za Wizara ikishirikiana na taasisi zilizochini ya Wizara.

v. Kufanya mapitio Sera ya Usafiri Zanzibar ili iendane sambamba na mabadiliko ya wakati pamoja na kutayarisha Sera ya Ujenzi itakayotoa Muongozo wa namna ya kuisimamia Sekta hiyo.

vi. Vilevile, Idara itaendelea kukusanya na kuchambua takwimu za maendeleo ya Sekta na kuweka Mpango bora wa utunzaji wa kumbukumbu za takwimu.

vii. Kuandaa Mpango Mkakati wa Takwimu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

viii. Kutayarisha na kuratibu mapitio ya Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali inayosimamia Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kuzifanyia marekebisho ili ziendane na mahitaji na mabadiliko yaliyopo kwa sasa.

ix. Kuendelea kuratibu na kuandaa vikao vya mashirikiano baina ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (SMZ), Wizara ya Ujenzi (SJMT), Wizara ya Uchukuzi (SJMT) pamoja na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (SJMT).

x. Kuratibu na kusimamia mashirikiano ya Kisekta, Kikanda na Kimataifa ikiwemo kushiriki mikutano mbalimbali inayoandaliwa kuhusu Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

xi. Kuendelea kuratibu na kusimamia Taasisi na Mashirika yanayojitegemea yaliyo chini ya Wizara hii.

**156. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara inaombewa kutumia jumla ya **Shilingi 1,128,908,000** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 506,958,000** ni mishahara na **Shilingi 621,950,000** ni matumizi mengineo.

**SP010403 - Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba**

**157. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamiwa na Ofisi Kuu Pemba na ina lengo la kuhakikisha majukumu ya Wizara yanatekelezwa ipasavyo kwa upande wa Pemba.

**158. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi Kuu Pemba kupitia Programu hii imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuimarisha mazingira bora ya kazi kwa watendaji ikiwemo kusimamia upatikanaji wa huduma muhimu za uendeshaji wa Ofisi, kufanya matengenezo ya Jengo la Ofisi, ununuzi wa Vifaa vya kufanyia kazi pamoja na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao .

ii. Kuwajengea uwezo watendaji kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi.

iii. Kuboresha Mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa Miradi mbali mbali ya Maendeleo inayoendelea kujengwa kwa Pemba.

iv. Kuendelea na ufuatiliaji na kusimamia kazi za miradi mbali mbali ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara kwa upande wa Pemba.

v. Kuendelea kutoa elimu ya TEHAMA kupitia vituo vya TEHAMA jamii kwa wananchi, kuratibu na kuendeleza matumizi ya Anuani za Makaazi na Postikodi, Kituo cha huduma kwa wateja pamoja na kuendelea kusimamia miundombinu ya TEHAMA kwa upande wa Pemba.

**159. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba inaombewa kutumia jumla ya **Shilingi 1,243,137,000** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 593,127,000** ni mishahara na **Shilingi 650,000,000** ni matumizi mengineyo.

## I. HITIMISHO

**160. Mheshimiwa Spika**, Kabla sijamaliza hotuba yangu hii sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu na ustahamilivu wakati wote nilipokua nikitoa maelezo ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Ni matumaini yangu kwamba Baraza lako Tukufu litatoa michango ambayo itasaidia Wizara kuendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo ya kuwahudumia wananchi wetu na hatimae kuipitisha Bajeti hii kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara zilizopangwa kwa kila Programu katika Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**161. Mheshimiwa Spika,** Pia naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena kumshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa moyo wake wa kupenda Amani na Maendeleo kwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema yeye na familia yake ili aendelee kutuongoza kwa mafanikio makubwa. Sote tunashuhudia kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Rais katika kuiletea maendeleo nchi yetu. Hivyo, sote tunawajibu wa kutekeleza usemi maarufu kwamba mcheza kwao hutunzwa.

**162. Mheshimiwa Spika,** Malengo na mafanikio ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ambayo nimeyaeleza kwa kina katika hotuba hii, ni matokeo ya ushirikiano wa wadau mbalimbali wa ndani na nje ya Nchi. Kwa niaba ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, napenda kuchukua fursa hii kuzitambua, kuzishukuru na kuzipongeza Taasisi mbalimbali tulizoshirikiana nazo katika kuendeleza Sekta mbalimbali za Wizara hii. Shukurani za dhati ziende kwa Washirika wa Maendeleo wakiwemo Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi Afrika (BADEA), Saudi Fund, United Kingdom Export Finance ya Uingereza, Benki ya Dunia na Mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwemo Shirika la Bahari Duniani (IMO), Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mawasiliano ( ITU ).

**163. Mheshimiwa Spika,** Vile vile, natoa shukurani zangu kwa Taasisi binafsi zinazotoa huduma za Mawasiliano na Usafirishaji hapa Zanzibar ikiwemo Kampuni za Mawasiliano za Yas, Halotel, Airtel, Vodacom, TTCL na Zanlink. Kwa upande wa Kampuni za Usafirishaji wa baharini tunazipongeza Kampuni za Azam Marine Company LTD, Zan Fast Ferries Company, Ikraam Sealine Company, Flying Shipping Company, Shirika la Meli Zanzibar pamoja na Kampuni ya Danaos inayotoa ajira ya ubaharia kwa wananchi wa Zanzibar.

Kwa upande wa Usafiri wa Anga tunazipongeza Kampuni za Air Tanzania, Assalam Air, Coastal Travel, Auric Air, Unity Air, Pelican Air, Precision Air, Zan Air, Regional Air, Flight link, My Fly Aviation, Safari Air Link, Air Excel, Tropical Air, Fly Zanzibar na Kampuni za Kimataifa ikiwemo Ethiopian Airlines, Sky Up Airline, Turkish Airlines, Qatar Airlines, Fly Dubai, Air France, Kenya Airways, Oman Air, Uganda Air, Israil Airlines, KLM Airlines, Condor Air, World 2 Fly, Fly One, Jambo Jet, Air Kenya na nyenginezo.

**164. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Usafiri wa Nchi Kavu tunawapongeza na kuwashukuru Wamiliki na Watendaji wa vyombo vya Usafiri wa Nchi Kavu ikiwemo Daladala, Magari ya Shamba, Bodaboda pamoja na Bajaji kwa mchango wao mkubwa wanaoutoa katika kufanikisha huduma za usafiri kwa wananchi.

Kwa upande wa Sekta ya Ujenzi, tunazipongeza Kampuni mbalimbali za ujenzi zinazofanya kazi Zanzibar pamoja na kuwashukuru Wataalamu wa ujenzi waliopo Zanzibar kwa mchango wao mkubwa katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.

**165. Mheshimiwa Spika,** Kampuni hizi zimechangia kwa kiasi kikubwa katika kuimarisha Sekta ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi hapa Zanzibar. Kwa niaba ya Serikali na kwa kupitia Baraza lako Tukufu noamba kutoa wito, kuwaomba wadau waliotajwa hapo juu na wengineo kuendelea kushirikiana na Serikali katika kutoa huduma za Usafirishaji, Ujenzi na Mawasiliano hapa Nchini.

**166. Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati Viongozi wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi nikianza na Mheshimiwa Nadir Abdulatif Alwardy Naibu Waziri ambae pia ni Mwakilishi wa kuchaguliwa na wananchi katika Jimbo la Chaani, Wenyeviti wa Bodi za Taasisi zilizochini ya Wizara hii, Katibu Mkuu Dkt. Habiba Hassan Omar, Naibu Katibu Mkuu (Ujenzi na Uchukuzi) Ndugu Makame Machano Haji, Naibu Katibu Mkuu (Mawasiliano) Ndugu Hawwah Ibrahim Mbaye, Afisa Mdhamini Ndugu Ibrahim Saleh Juma, Ndugu Mahfoudh M. Hassan Mkurugenzi Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Ndugu Issa Sarboko Makaran Mkurugenzi Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

